JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC)

TAARIFA YA KAMATI KUHUSU RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA HESABU ZILIZOKAGULIWA ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MIAKA YA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025

(Inatolewa chini ya Kanuni ya 139 (16) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Mwaka 2025)

3 NOVEMBA, 2026

DIBAJI

Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa niaba ya Bunge imekuwa ikishughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025. Utekelezaji wa majukumu ya Bunge unafanyika kwa kupitia na kuchambua Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Taarifa hii imejumuisha uchambuzi wa maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma na matokeo ya uchambuzi huo, maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka miwili ya fedha 2023/2024 na 2024/2025. Maeneo yaliyobainika kuwa na mapungufu ni pamoja na baadhi ya Halmashauri kukosa mipango madhubuti ya ukusanyaji wa mapato ya ndani na kusababisha utegemezi wa Ruzuku ya Serikali kufikia **Asilimia 83**.

Kwa upande wa uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Serikali, Kamati imebaini ukiukwaji wa matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na Kanuni zake kwa baadhi ya Halmashauri na mapungufu katika usimamizi wa Mikataba. Changamoto ya ukiukwaji wa Sheria na Kanuni za kutenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo na Mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu imeendelea kuonekana katika Halmashauri nyingi kwa kila mwaka wa ukaguzi.

Kamati pia imebaini mapungufu katika usimamizi wa Ardhi ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Kibaha na Halmashauri ya Jiji la Tanga zimebainika kukiuka taratibu za ugawaji na uuzaji wa viwanja katika maeneo yao. Pamoja na hayo, Kamati imebaini Halmashauri nyingi kutekeleza miradi katika maeneo ambayo hawana Hati Miliki na Mali za Halmashauri kutoingizwa kwa usahihi katika Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS).

Udhaifu wa mifumo ya ndani katika usimamizi wa miradi umesababisha Halmashauri ya Jiji la Mwanza kutokamilisha ujenzi wa Ofisi za Idara za Afya kwa takriban miaka 14. Vile vile, baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikidaiwa fidia ya Ardhi yenye jumla ya **Sh. Bilioni 28.76**.

Uchambuzi wa hoja zote umefanyika kwa ufanisi na weledi ili kuhakikisha kunakuwa na mnyororo thabiti wa uwajibikaji kwa waliopewa dhamana ya matumizi ya fedha za Umma kwa niaba ya wananchi. Aidha, Mapendekezo ya Kamati katika maeneo yote yanalenga kurekebisha dosari zote zilizobainika ili Halmashauri zote 184 ziwe na matumizi mazuri ya fedha za Umma.

YALIYOMO

Ukurasa

DIBAJI ..... **I**

ORODHA YA MAJEDWALI ..... **V**

SEHEMU YA KWANZA **1**

1.0 MAELEZO YA JUMLA **1**

1.1 UTANGULIZI 1
1.2 MUUNDO WA TAARIFA 2
1.3 MAJUKUMU YA KAMATI 3
1.4 NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA KUTEKELEZA MAJUKUMU YA KAMATI 3
1.5 MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI 6
1.6 UFUATILIAJI WA MAPENDEKEZO YALIYOTOLEWA NA KAMATI 7
1.7 UFUATILIAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE 7

SEHEMU YA PILI **8**

2.0 UCHAMBUZI WA RIPOTI KUU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI YA UKAGUZI WA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MIAKA MIWILI YA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025 ..... **8**

2.1 MAELEZO YA JUMLA 8
2.2 VIGEZO VYA UCHAMBUZI 9
2.3 MATOKEO YA UCHAMBUZI 11
2.3.1 Usimamizi usioridhisha katika Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri 12
2.3.1.1 Kutofikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri 14
2.3.1.2 Kukosekana kwa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na kusababisha upotevu wa Sh. Bilioni 5.34 17
2.3.1.3 Mapato yasiyokusanywa kutoka Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) 18
2.3.1.4 Mapato yanayotokana na Ushuru wa Huduma yasiyokusanywa Sh. Bilioni 8.52 19
2.3.1.5 Mawakala wa ukusanyaji wa Mapato kutowasilisha Sh. Bilioni 13.34 21
2.3.1.6 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutowasilisha Halmashauri Marejesho ya 20% ya Kodi ya Ardhi Sh. Bilioni 13.54 22
2.3.1.7 Kutohuishwa kwa kanzi data ya walipa kodi katika Halmashauri 23
2.3.1.8 Upotevu wa Mapato unaotokana na Mashauri kuwa TAKUKURU kwa muda Mrefu 25
2.3.2 Matumizi ya Fedha za Umma kinyume na Sheria na Kanuni pamoja na usimamizi usioridhisha wa Akaunti ya Amana 27
2.3.3 Ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na mapungufu katika usimamizi wa Mikataba 33
2.3.4 Madeni ya Halmashauri kutolipwa kwa wakati (Payables) 44
2.3.5 Mapungufu katika utekelezaji wa miradi ya Maendeleo 50
2.3.6 Mapungufu katika Usimamizi wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu 66

2.3.7 Kukosekana kwa mipango sahihi ya uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 73
2.3.7.1 Changamoto za Uwekezaji katika Masoko 74
2.3.8 Usimamizi Usioridhisha wa Rasilimali watu 81
2.3.8.1 Changamoto za Kiutendaji katika Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani 82
2.3.8.2 Halmashauri kuwa na wakuu wa Idara na Vitengo wasio na Sifa na Wanaokaimu kwa muda mrefu 84
2.3.8.3 Michango ya watumishi kutowasilishwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) 86
2.3.9 Kukosekana kwa Udhibiti katika Usimamizi wa Mali za Umma 87
2.3.9.1 Kutokuwepo kwa Matumizi Sahihi ya Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS) 88
2.3.9.2 Kukosekana kwa Mpango Rasmi wa Matengenezo na Uondoshaji wa Mali Chakavu 90
2.3.10 Changamoto katika Usimamizi wa Ardhi 91
2.3.11 Utekelezaji usioridhisha wa Mapendekezo ya Kamati na Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali 97
2.3.11.1 Utekelezaji Usioridhisha wa Mapendekezo ya Kamati 97
2.3.11.2 Utekelezaji Usioridhisha wa Hoja na Mapendekezo ya CAG 99
SEHEMU YA TATU 101

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO 101

3.1 MELEZO YA JUMLA 101
3.2 MAONI 101
3.3 MAPENDEKEZO 104
3.3.1 Usimamizi Usioridhisha katika Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri 104
3.3.2 Matumizi ya Fedha za Umma Kinyume na Sheria na Kanuni pamoja na Usimamizi Usioridhisha wa Akaunti ya Amana 106
3.3.3 Ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na Mapungufu katika Usimamizi wa Mikataba 106
3.3.4 Madeni ya Halmashauri Kutolipwa kwa Wakati 107
3.3.5 Mapungufu katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo 108
3.3.6 Mapungufu katika Usimamizi wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu 109
3.3.7 Kukosekana kwa Mipango Sahihi ya Uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 110
3.3.8 Usimamizi Usioridhisha wa Rasilimali Watu 111
3.3.9 Kukosekana kwa Udhibiti katika Usimamizi wa Mali za Umma 112
3.3.10 Changamoto katika Usimamizi wa Ardhi 113
3.3.11 Utekelezaji Usioridhisha wa mapendekezo ya Kamati na Hoja na Mapendekezo yote yaliyotolewa katika taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa 114
SEHEMU YA NNE 116

4.0 HITIMISHO 116

1.1 HITIMISHO 116
4.1 HOJA 118

ORODHA YA MAJEDWALI

JEDWALI NA. 1: HALMASHAURI ZILIZOSHINDWA KUFIKIA MALENGO YA UKUSANYAJI WA MAPATO KWA MWAKA 2023/2024.....15
JEDWALI NA. 2: HALMASHAURI ZILIZOSHINDWA KUFIKIA MALENGO YA UKUSANYAJI WA MAPATO KWA MWAKA 2024/2025.....16
JEDWALI NA. 3: HALMASHAURI ZINAZOIDAI WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI.....23
JEDWALI NA. 4: MADENI YA WATUMISHI YANAYOPASWA KULIPWA NA SERIKALI KUU ZAIDI YA BILIONI MOJA.....45
JEDWALI NA. 5: MADENI YA WATUMISHI YANAYOPASWA KULIPWA NA HALMASHAURI ZAIDI YA BILIONI MOJA.....46
JEDWALI NA. 6: HALMASHAURI ZILIZOTENGA BAJETI PUNGUFU YA ULIPAJI WA MADENI.....46
JEDWALI NA. 7: MADENI YA WAZABUNI YANAYOPASWA KULIPWA NA SERIKALI KUU ZAIDI YA MILIONI MIA TANO.....48
JEDWALI NA. 8: MADENI YA WAZABUNI YANAYOPASWA KULIPWA NA HALMASHAURI ZAIDI YA BILIONI MOJA.....49
JEDWALI NA. 9: ORODHA YA HALMASHAURI AMBAO HAZIJAKAMILISHA MIRADI KWA WAKATI.....52
JEDWALI NA. 10: HALMASHAURI AMBAZO HAZIKUPELEKA FEDHA ZOTE ZA MIRADI YA MAENDELEO KUTOKA KATIKA MAPATO YA NDANI.....63
JEDWALI NA. 11: KAMPUNI ZISIZOTEKELEZA WAJIBU KWA JAMII (CSR).....64
JEDWALI NA. 12: HALMASHAURI AMBAZO HAZIKUCHANGIA KIKAMILIFU KATIKA MFUMO WA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU KWA MIAKA MITATU (2022/2023 HADI 2024/2025) **.....67**
JEDWALI NA. 13: HALMASHAURI AMBAZO HAZIJAKUSANYA MIKOPO ILIYOTOLEWA KATIKA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU ZAIDI YA BILIONI 1.....69
JEDWALI NA. 14: HALMASHAURI AMBAZO HAZIKUZINGATIA UWIANO WA 4:4:2.....71
JEDWALI NA. 15: HALMASHAURI ZILIZOZIDISHA FEDHA ZA UFUATILIAJI 2024/2025.....73
JEDWALI NA. 16: IDADI YA WAKUU WA IDARA NA VITENGO WANAOKAIMU KWA MUDA MREFU.....85
JEDWALI NA. 17: HALMASHAURI AMBAZO HAZIKUWASILISHA MICHANGO YA WATUMISHI KATIKA MFUKO WA PSSSF....87
JEDWALI NA. 18: HALMASHAURI AMBAZO HAZIJATEKELEZA KIKAMILIFU MAPENDEKEZO YA KAMATI.....98
JEDWALI NA. 19: HALMASHAURI AMBAZO HAZIJATEKELEZA KIKAMILIFU MAPENDEKEZO YA CAG KWA KIASI KIKUBWA **100**

TAARIFA YA KAMATI KUHUSU RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA HESABU ZILIZOKAGULIWA ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MIAKA YA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025

_____

(Inatolewa chini ya Kanuni ya 139 (16) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025)

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 pamoja na Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2025 na kuliomba Bunge liipokee na kuijadili. Madhumuni ya Taarifa hii ni kulijulisha Bunge lako tukufu juu ya matumizi ya fedha za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na iwapo matumizi hayo yamezingatia Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali ya nchi na kuleta manufaa na tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi mazuri ya fedha za umma, Taarifa hii inafafanua Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka miwili 2023/2024 na 2024/2025.

Uchambuzi umejikita katika kubainisha dosari zilizopo katika matumizi ya fedha za umma ikijumuisha ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo inayopaswa kufuatwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

1.2 Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 145 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025 imeweka sharti la muundo wa Taarifa inayowasilishwa Bungeni. Kanuni hii imefafanua kuwa, Taarifa yoyote ya Kamati inapaswa kuwa na sehemu kuu tatu zikihitimishwa na sehemu ya nne yenye shukrani na utoaji wa hoja. Ili kuwa na mtiririko mzuri wa ufuatiliaji wa taarifa hii, sehemu ya kwanza ni ya utangulizi ambayo itaonesha hadidu za rejea, maelekezo yoyote yaliyotolewa kwa Kamati, njia au mbinu zilizotumika na kamati katika kutekeleza majukumu yake na masuala mengine yaliyojitokeza kama yapo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili itatoa maelezo kamili kuhusu jambo lililofanyiwa kazi na Kamati ambapo, uchambuzi wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa na matokeo ya uchambuzi huo unaoonesha matumizi mabaya ya fedha za umma kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na 2024/2025 umefanunuliwa katika sehemu ya Pili ya Taarifa hii ambayo inajenga msingi wa sehemu ya Tatu inayohusu Maoni na Mapendekezo.

1.3 Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati yamefafanuliwa katika Kifungu cha 14 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025. Kwa mujibu ya Kanuni hii, majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ni yafuatayo: -

a) Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ili kuondoa matatizo hayo; na

c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Serikali za Mitaa kuhusu matumizi mazuri ya fedha ili kuhakikisha kwamba, tatizo la matumizi mabaya ya fedha za Umma linapungua.

Mheshimiwa Spika, Msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 15 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge ya Mwaka 2025.

1.4 Njia zilizotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kama ilivyobainishwa katika Kanuni ya 145 (a) (iii) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, naomba kutaja njia na mbinu zilizotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati na kukamilisha Taarifa hii kama ifuatavyo: -

a) Mapitio ya jumla ya Ripoti Kuu ya Mwaka ya CAG kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka miwili ya fedha 2023/2024 na 2024/2025. Uchambuzi wa Ripoti hizi hubainisha maeneo yenye matatizo katika mapato na matumizi ya fedha za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha husika na iwapo kama kuna ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na miongozo;

b) Kupokea Taarifa fupi za CAG (*Briefs*) ambazo huonesha utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati, Hoja za ukaguzi na Mapendekezo ya CAG kuhusu Hesabu za Halmashauri husika. Taarifa hizi huwaweka Wajumbe wa Kamati katika nafasi nzuri ya kuzielewa hoja kwa undani wake na kubaini maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma ili kuweza kuishauri na kuisimamia Serikali ipasavyo;

c) Mahojiano na Wakurugenzi wa Halmashauri kuhusu hoja zilizobainishwa katika Ripoti ya CAG ili kubaini kigezo cha upatikanaji wa hoja, hali halisi iliyopo inayopaswa kujadiliwa na Kamati, chanzo, sababu au chimbuko la hoja pamoja na athari zinazotokana na hoja husika; na

d) Uchambuzi wa kina wa Taarifa za wakaguzi, majibu ya Wakurugenzi wa Halmashauri iliyokaguliwa pamoja na mashauriano na Wadau wengine kuhusu hoja za Ukaguzi zilizojitokeza. Lengo ni kuelewa kwa kina msingi wa hoja na namna ya kupunguza matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, njia na mbinu zilizotumiwa na Kamati, ziliiwezesha Kamati kufanya uchambuzi wa kina wa Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa za Halmashauri kwa lengo la kulishauri Bunge hatua za kuchukua ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika kukamilisha kazi hiyo, Kamati ilifanya rejea ya Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali kama ifuatavyo: -

a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977;

b) Sheria ya Ukaguzi wa Umma (Sura ya 418) na Kanuni zake za Mwaka 2009;

c) Sheria ya Fedha za Halmashauri (Sura ya 290) na Mwongozo wa Matumizi ya fedha katika Serikali za Mitaa (*the Local Government Financial Memoranda*);

d) Sheria ya Ununuzi wa Umma (Sura ya 410) na Kanuni zake, (kama zilivyo boreshwa mwaka 2023);

e) Sheria ya Bajeti (Sura ya 439) na Kanuni zake, 2015;

f) Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki ya Bunge, Sura 296;

g) Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025; na

h) Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009.

1.5 Muhtasari wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, baada ya Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilishwa Bungeni kama ilivyotamkwa katika Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, ripoti zinazohusu Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa hujadiliwa na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa niaba ya Bunge.

Kwa muktadha wa utekelezaji wa matakwa ya Ibara hiyo, tarehe 10 Aprili, 2026 Serikali iliweka mezani Ripoti mbalimbali za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Miongoni mwa Ripoti hizo ilikuwa ni Ripoti Kuu ya Mwaka ya Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025.

Ripoti zilizowasilishwa ni zao la kukamilika kwa jukumu la kikatiba la Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kama ilivyotamkwa katika Ibara ya 143 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Katika kipindi cha miaka miwili ya fedha (2023/2024 na 2024/2025) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alifanya ukaguzi na kutoa ripoti katika jumla ya Mamlaka 184 za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika kuitekeleza dhima ya Bunge ya kuisimamia Serikali, Kamati ilichambua na kujadili Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa na kufanya mahojiano na Wakurugenzi wa **Halmashauri 75** ambazo ni sawa na **Asilimia**

40.76 ya Halmashauri zote 184 ambazo Hesabu zake zimekaguliwa. Shughuli hiyo ilifanyika ili kufuatilia nidhamu ya mapato na matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kwamba, kunakuwa na matumizi mazuri ya fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa kina wa hoja zilizochambuliwa na Kamati umefafanuliwa katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

1.6 Ufuatiliaji wa Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 14 (b) ya Nyongeza ya Nane ya kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, Kamati imekuwa ikifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati katika vikao vilivyopita. Zoezi hilo hufanyika kupitia '*briefs'* za CAG kwa kila Halmashauri inayofika mbele ya Kamati kwa ajili ya Mahojiano.

1.7 Ufuatiliaji wa Maazimio ya Bunge

Mheshimiwa Spika, baada ya Taarifa ya Kamati kuwasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni ya 139 (16) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, na Mapendekezo ya Kamati kuafikiwa na Bunge zima na hatimaye kuwa ni Maazimio ya Bunge, Kamati ina jukumu lingine la kufuatilia utekelezaji wa Maazimio hayo. Jukumu hilo lililobainishwa katika Kanuni ya 139 (17) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025 linadhamiria kuhakikisha Serikali inatekeleza kikamilifu Maazimio yote yaliyotolewa na Bunge.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA RIPOTI KUU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI, KUHUSU UKAGUZI WA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MIAKA MIWILI YA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025

2.1 Maelezo ya jumla

Mheshimiwa Spika, Madaraka na Majukumu ya Bunge yameelezewa katika Ibara ya 63 na 64 ya Katiba. Madaraka hayo yamefafanuliwa zaidi katika Ibara ya 63 (2)(3) ya Katiba kuwa ni kuisimamia na kuishauri Serikali na vyombo vyake vyote kwa niaba ya Wananchi. Kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa madaraka haya, Bunge hukasimisha baadhi ya majukumu yake kwa Kamati za Bunge ambapo uwepo wa Kamati hizo ni kwa mujibu wa Ibara ya 96 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977).

Utekelezaji wa matakwa ya Katiba pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge unalenga kuimarisha mnyororo wa uwajibikaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hasa katika matumizi ya fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha iwapo matumizi ya fedha za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yamezingatia Sheria, Kanuni na Miongozo, Ibara ya 143 (2) ya Katiba imempa CAG ambaye ndiye jicho la Bunge mamlaka ya kutekeleza majukumu yake kwa niaba ya Bunge.

Katika kuhakikisha mapendekezo yaliyotolewa na CAG katika ripoti zake yanatekelezwa kikamilifu, Kamati ilichambua Ripoti Kuu ya Mwaka ya CAG kuhusu Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuhusu uchambuzi wa Ripoti za CAG ambazo ndio msingi wa mapendekezo ya Kamati yanayowasilishwa kwa njia ya Hoja kama ilivyoelekezwa na Kanuni ya 63 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

2.2 Vigezo vya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Ripoti za CAG zilizofanyiwa kazi na Kamati zinajumuisha hoja na mapendekezo ya Halmashauri zote zilizokaguliwa katika mwaka husika. Uchambuzi wa Hesabu zilizokaguliwa (individual report) kwa kila Halmashauri ulitokana na vigezo ambavyo Kamati imejiwekea ili kuhakikisha kunakuwa na ufanisi wakati wa kushughulikia utekelezaji wa hoja na mapendekezo ya CAG ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma.

Vigezo vilivyowekwa viliisaidia Kamati kuainisha maeneo ya kipaumbele ya kufanyiwa uchambuzi katika Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa (*individual financial statements*) na Maafisa Masuuli

(Wakurugenzi) wa Halmashauri hizo walifika mbele ya Kamati kwa ajili ya mahojiano.

Mheshimiwa Spika, vigezo muhimu vilivyozingatiwa na Kamati wakati wa uchambuzi wa Ripoti za CAG ni kama ifuatavyo: **-**

a) Uzito wa hoja ya ukaguzi kama ilivyoibuliwa na CAG;

b) Maslahi ya Umma kuhusu hoja za Halmashauri husika;

c) Hali ya hati ya ukaguzi iliyotolewa kwa Halmashauri husika;

d) Kujirudia mara kwa mara kwa hoja husika katika Halmashauri au Mradi wa Maendeleo uliokaguliwa;

e) Kiwango cha fedha kinachohusika katika hoja za ukaguzi wa Halmashauri husika; na

f) Kuleta uendelevu wa ufuatiliaji wa ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati kwa Halmashauri husika kwa siku za nyuma.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Ripoti za CAG kwa kutumia vigezo vilivyoainishwa uliiwezesha Kamati kufikia malengo yake kwa kubainisha maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za Umma na hatimaye kutoa mapendekezo stahiki.

2.3 Matokeo ya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, kwa miaka miwili 2023/2024 na 2024/2025, Ukaguzi wa CAG ulifanyika katika jumla ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri) 184. Matokeo ya ukaguzi huo yalipelekea kutolewa kwa hati za ukaguzi kwa Halmashauri zote 184. Hati zilizotolewa zilitokana na tathmini ya ukaguzi na kuangalia iwapo taarifa za fedha zilizingatia mifumo husika ya utoaji wa taarifa za fedha.

Katika Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024, Halmashauri zote 184 zilipata Hati zinazoridhisha za ukaguzi. Aidha, kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2025, Halmashauri 182 sawa na **Asilimia 98.91** zilipata Hati zinazoridhisha za Ukaguzi na Halmashauri 2 sawa na **Asilimia 1.09** zilipata Hati zenye shaka za ukaguzi.

Uchambuzi wa Kamati uliofanywa katika Ripoti Kuu ya CAG ulibaini kuwa, idadi ya Halmashauri zilizopata Hati zinazoridhisha zimepungua kutoka Halmashauri 184 kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 hadi Halmashauri 182 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, Kwa upande wa Hati zenye shaka, Mwaka wa Fedha 2024/2025 Halmashauri 2 zimepata Hati yenye shaka wakati Mwaka 2023/2024 hapakuwa na Hati yenye shaka.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati wa Hesabu za Serikali za Mitaa katika ripoti zote mbili ulijikita katika maeneo kadhaa

yenye matumizi mabaya ya fedha za umma ambayo ni ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Serikali ikiwa ni pamoja na kutochangia mapato ya ndani ya Halmashauri katika miradi ya maendeleo na Mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, Halmashauri kukosa mikakati ya ukusanyaji wa mapato ya ndani pamoja na Halmashauri nyingi kutolipa madeni ya watumishi na wazabuni.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya utangulizi ya sehemu hii ya pili, mambo yafuatayo kuhusu matumizi na usimamizi wa fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yalibainika: -

2.3.1 Usimamizi usioridhisha katika Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri

Mheshimiwa Spika, Eneo la ukusanyaji wa mapato ni kiini cha utekelezaji wa majukumu ya Halmashauri zote nchini, uchambuzi wa Kamati ulijikita katika kuangalia usimamizi wa fedha za umma na utayari wa Halmashauri zote nchini kuongeza uwezo wa kukusanya ili ziweze kujiendesha na kupunguza utegemezi wa fedha za Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikipeleka fedha nyingi katika Halmashauri zote nchini zikiwa ni fedha kwa ajili ya maendeleo, mishahara na matumizi ya kawaida. Hata hivyo, Kamati imebaini Halmashauri nyingi nchini kukosa mikakati madhubuti ya kuongeza mapato ya ndani na kuendelea kutegemea ruzuku ya Serikali kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali ilipeleka fedha za ruzuku jumla ya **Sh. 6,937,298,388,464** katika Halmashauri zote 184 ambapo kati ya fedha hizo, **Sh. 1,339,146,090,639** zilikuwa ni ruzuku za matumizi ya maendeleo na **Sh. 5,659,691,586,276** zilikuwa ni ruzuku kwa ajili ya mishahara na matumizi ya kawaida. Pamoja na kiasi kikubwa cha fedha kilichotolewa na Serikali Kuu, ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa Halmashauri zote nchini haukuwa ni wenye kuridhisha kwakuwa, kiasi cha **Sh. 1,465,008,536,533** pekee ndicho kilichokusanywa na Halamashauri zote 184.

Kutokana na takwimu hizo za jumla, Halmashauri zinapaswa kuwa na mikakati madhubuti ya kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kubuni vyanzo vipya endelevu vya mapato na kuhakikisha vyanzo vya mapato vilivyopo vinakusanywa kikamilifu pamoja na kuziba mianya ya upotevu wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Halmashauri nyingi kushindwa kukusanya mapato ya kutosha, Taarifa ya CAG kwa mwaka wa fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2025 zilizonesha kuwa, utegemezi wa ruzuku ya Serikali kwa ujumla ni **Asilimia 83** ambapo, Halmashauri zinategemea ruzuku kwa ajili ya mishahara na matumizi ya kawaida kwa **Asilimia 79** na utegemezi wa ruzuku kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ni **Asilimia 48**. Takwimu hizi zinaonesha ni kwa kiasi gani Halmashauri zinapaswa kuwa na mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa mapato ili kupunguza utegemezi wa ruzuku ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri 75 zilizofika mbele ya Kamati, Serikali ilipeleka ruzuku ya jumla ya **Sh. 1,003,696,991,488.89** Kwa ajili ya matumizi ya maendeleo na **Sh. 2,451,395,801,464.67** Kwa ajili ya ruzuku ya mishahara na matumizi ya kawaida. Kwa upande wa makusanyo ya mapato ya ndani, Halmashauri hizo 75 zilikusanya jumla ya **Sh. 670,696,398,170.37**. Mchanganuo wa upokeaji wa ruzuku ya Serikali ikilinganishwana na ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa Halmashauri zote 75 ni **kiambatisho namba 1** cha Taarifa hii.

Baada ya uchambuzi wa kina wa Kamati, changamoto nyingine zilizobainika katika usimamizi wa mapato ya ndani ya Halmashauri ni kama ifuatavyo:-

2.3.1.1 Kutofikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikifuatilia mtiririko wa makusanyo ya mapato kutoka vyanzo vya mapato ya ndani vya Halmashauri ili kujiridhisha iwapo Halmashauri zinakusanya mapato kama zilivyoainisha katika bajeti zao ambazo zimeidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Halmashauri nyingi hazifikii malengo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kinyume na maelekezo ya Kipengele cha 4.2.2 cha Mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya Serikali wa Mwaka

2024/2025 ulioandaliwa kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Sura 439 na Kanuni zake 2015.

Hali hiyo inatokana na kukosekana kwa ubunifu wa vyanzo vipya vya mapato ambavyo ni endelevu na kushindwa kukusanya kikamilifu katika vyanzo vilivyopo pamoja na kutoziba mianya ya upotevu wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ya Halmashauri kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji ni wakusanya mapato kutofikia kiwango cha ukusanyaji kilichoafikiwa katika mikataba ya ukusanyaji pamoja na kukosekana kwa taarifa sahihi za mauzo ghafi ya wafanyabiashara wakubwa waliopo katika Halmashauri hizo hivyo kupelekea kukusanywa kwa kiasi kidogo cha mapato.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2023/2024 baadhi ya Halmashauri zilizoshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa zaidi ya **Asilimia Kumi** ni kama inavyoonekana katika jedwali namba 1.

Jedwali Na. 1: Halmashauri Zilizoshindwa kufikia Malengo ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka 2023/2024

Jina la Halmashauri	Bajeti iliyoidhinishwa	Makusanyo halisi	Pungufu	Asilimia
H/W Bariadi	Sh. 3,050,954,664.00	Sh. 2,339,273,022.00	Sh. 711,681,642.00	23
H/W Pangani	Sh. 1,947,973,000.00	Sh. 1,523,721,106.00	Sh. 424,251,894.00	22
H/Jiji Arusha	Sh. 48,979,752,000.00	Sh. 37,977,671,908.00	Sh. 11,002,080,092.00	22
H/W Njombe	Sh. 5,208,011,760.00	Sh. 4,130,369,992.00	Sh. 1,077,641,768.00	21
H/W Kishapu	Sh. 4,583,027,514.00	Sh. 3,788,056,301.00	Sh. 794,971,213.00	17

Jina la Halmashauri	Bajeti iliyoidhinishwa	Makusanyo halisi	Pungufu	Asilimia
H/Jiji Tanga	Sh. 19,145,700,000.00	Sh. 16,257,618,490.00	Sh. 2,888,081,510.00	15

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2024/2025 baadhi ya Halmashauri zilizoshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa zaidi ya **Asilimia Kumi** ni kama inavyoonekana katika Jedwali namba 2.

Jedwali Na. 2: Halmashauri zilizoshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa Mwaka 2024/2025

Jina la Halmashauri	Bajeti iliyoidhinishwa	Makusanyo Halisi	Pungufu	Asilimia
H/Jiji Tanga	Sh. 21,060,270,000.00	Sh. 15,021,383,800.00	Sh. 6,038,886,200.00	29
H/M Musoma	Sh. 5,308,223,000.00	Sh. 4,515,164,690.00	Sh. 793,058,310.00	15
H/W Misungwi	Sh. 4,704,013,000.00	Sh. 4,022,887,950.00	Sh. 681,125,050.00	14
H/W Bunda	Sh. 2,521,286,000.00	Sh. 2,195,383,847.00	Sh. 325,902,153.00	13
H/M Singida	Sh. 6,767,656,000.00	Sh. 5,981,265,311.00	Sh. 786,390,689.00	12

Mheshimiwa Spika, Halmashauri kushindwa kukusanya mapato ya ndani kunaathiri utekelezaji wa shughuli za kila siku pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kusababisha upotevu wa fedha za Umma. Maelezo ya baadhi ya Maafisa Masuuli waliofika mbele ya Kamati hayakuonesha nia thabiti ya kufanya upembuzi wa kina wa namna bora ya ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha uwezo wa kifedha wa Halmashauri zote nchini, Kamati imekuwa ikizielekeza Halmashauri zilizofika kwa ajili ya mahojiano kuhakikisha vyanzo vyote vya mapato vinafanya kazi kwa ufanisi kama ilivyopangwa na kuzuia mianya yote ya upotevu wa fedha za umma.

2.3.1.2 Kukosekana kwa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na kusababisha upotevu wa Sh. Bilioni 5.34

Mheshimiwa Spika, Aya ya 7.5.3 (ii–iv) ya Mwongozo wa Utawala wa Mapato wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2019 unazitaka Halmashauri kutambua watu binafsi na taasisi zote zinazotakiwa kutoa tozo za huduma, kuhakikisha ukusanyaji wenye ufanisi wa mapato, kuweka kumbukumbu sahihi za huduma zote zinazotozwa, na kuweka pamoja na kuhuisha takwimu za mapato kwa kila chanzo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikipoteza mapato yake kwa kushindwa kuwa na ufanisi katika ukusanyaji wa tozo mbalimbali, ushuru wa mazao, na mapato ya pango kutoka kwenye vizimba vya masoko. Kushindwa kukusanywa kwa mapato hayo kunapunguza ukwasi wa Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato kumesababisha H/W Mbozi kutokusanya mapato yenye jumla ya **Sh. 165,790,000** yanayotokana na vibanda vya soko la vwawa na **Sh. 207,715,920** za mapato ya Kahawa. Vile vile, H/Jiji Dodoma haikukusanya **Sh. 108,218,000** yanayotokana na maduka na vibanda katika masoko mbalimbali. Aidha, H/M Kigoma Ujiji ilishindwa

kukusanya **Sh.32,000,000** ambayo ni kodi ya miezi Nane kwa ajili ya upangishaji wa Jengo la Biashara la Kigoma Na. K.151, linalojulikana pia kama "KIGODECO" kutoka kwa Mfanyabiashara M/s Kigoma Catering and Food Supplies.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Masuuli wameieleza Kamati kuwa, juhudi za ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri zinaendelea. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuzisisitiza Halmashauri zote nchini kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato kwakuwa, kukosekana kwa fedha hizo kunapunguza uwezo wa kifedha wa Halamshauri husika na ni upotevu wa fedha za Umma.

2.3.1.3 Mapato yasiyokusanywa kutoka Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)

Mheshimiwa Spika, jukumu kuu la Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ni kuhakikisha usalama, utoshelevu, na uwepo wa akiba ya chakula cha kutosha kwa ajili ya Taifa. Pamoja na mambo mengine, jukumu lingine ni kununua mazao na nafaka za chakula (kama vile mahindi) moja kwa moja kutoka kwa wakulima nchini kwa bei elekezi ili kuwasaidia kupata soko.

Ukaguzi wa CAG umebaini uwepo madeni ambayo NFRA inadaiwa na baadhi ya Halmashauri ambazo ni fedha za ushuru wa mazao. Licha ya Halmashauri kufanya ufuatiliaji, bado fedha hizo hazijakusanywa na Halmashauri hizo. Kwa Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati ambazo zinaidai NFRA jumla ya **Sh. 2,916,960,362.00** ni pamoja na H/M Sumbawanga **Sh. 1,288,109,416.00**, H/M Songea **Sh.**

520,537,682.00, H/W Nachingwea **Sh. 341,682,377.00**, H/W Nkasi **Sh. 295,489,429.00**, H/W Madaba **Sh. 184,181,450.00**, H/W Namtumbo **Sh. 172,028,637.00** na H/Mji Makambako **Sh. 114,931,371.00**.

Mheshimiwa Spika, kutokusanywa kwa fedha hizo kunapunguza mapato ya Halmashauri pamoja na uwezo wa Halmashauri kuhudumia wananchi wake kikamilifu. Kamati inaitaka NFRA kuhakikisha inalipa madeni yake yote kwa wakati kama ambavyo ilikubaliana na Halmashauri husika.

2.3.1.4 Mapato yanayotokana na Ushuru wa Huduma yasiyokusanywa Sh. Bilioni 8.52

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa imeeleza kuwa, Mashirika/Taasisi/Kampuni au mtu yoyote anayefanya biashara iliyosajiliwa ambaye mauzo yake ya mwaka yanazidi **Sh Milioni 4** anapaswa kuilipa Halmashauri ushuru wa huduma (service levy) kwa kiwango kisichozidi **Asilimia 0.3** ya mauzo (turnover) baada ya kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na ushuru wa bidhaa.

Hata hivyo, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, kuna Halmashauri ambazo hazikukusanya jumla ya **Sh. 8,529,842,605** unaotokana na ushuru wa huduma kutoka kwa wafanyabiashara waliopo katika maeneo yao ya usimamizi. Kiasi hiko kimeongezeka kutoka **Sh. 8,098,377,896** zilizoripotiwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, kutokukusanywa kwa fedha hizo kunasababisha upotevu wa mapato ya Halmashauri. Aidha, kuongezeka kwa fedha ambazo hazijakusanywa kutoka **Bil 8.10** hadi **Bil 8.52** kunaashiria kuwa, hatua madhubuti za kuimarisha ukusanyaji wa mapato hazikuchukuliwa.

Mfano wa Halmashauri ambazo hazijakusanya ushuru wa Huduma ni H/W Sikonge (fedha za ushuru wa tumbaku) **Sh. 137,141,532.36**, na H/M Shinyanga haikukusanya **Sh. 136,337,240** kutoka katika Makampuni yaliyopewa bili. Kampuni 25 zinazofanya kazi katika migodi ya dhahabu ya Bulyanhulu katika H/W Msalala hazikulipa ushuru wa huduma wenye jumla ya **Sh. 94,091,154.96**.

Mheshimiwa Spika, Mfano mwingine ni H/W Tarime kutokusanya ushuru wa huduma kutoka kwa kampuni zinazotoa bidhaa na huduma kwa Mgodi wa Dhahabu wa North Mara **Sh. 421,180,538**. Vile vile, H/W Mbozi haikukusanya tozo ya ushuru wa kahawa kutoka kwa wamiliki wa mashamba makubwa ya Kahawa na AMCOS **Sh. 207,715,920**.

Mheshimiwa Spika, kinyume na Kifungu cha 6(1)(n) na 7(1) (aa) cha Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za mitaa Sura ya 290 na mbali na kiasi ambacho hakikukusanywa kilichotajwa hapo awali, **Makampuni 8,771** hayakulipa ushuru wa huduma kwa mwaka 2024/2025. Pamoja na idadi hiyo ya Makampuni kupungua kutoka Makampuni/Taasisi **29,432** zilizoripotiwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, jitihada za makusudi zinahitajika ili Kampuni zote zilipe ushuru wa huduma kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kwa Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati, H/W Msalala Makampuni 58 na H/W Kishapu Makampuni 29. Kamati inazitaka Halmashauri zote nchini kuweka mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa ushuru wa huduma ili kuongeza mapato ya Halmashauri zao.

2.3.1.5 Mawakala wa ukusanyaji wa Mapato kutowasilisha Sh. Bilioni 13.34

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zimekuwa zikiingia mikataba na Mawakala wa ukusanyaji wa mapato ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji, kuziba mianya ya upotevu wa fedha, kuruhusu matumizi ya vifaa vya kisasa na mifumo bora ya kidijitali ya ukusanyaji Pamoja na kupunguza udanganyifu.

Kinyume na matakwa ya Kifungu cha 29(2)(c) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, Mawakala wa ukusanyaji wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wamekuwa wakiwasilisha katika Halmashauri mapato chini ya kiasi kilichoainishwa katika mikataba yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, kutowasilishwa kwa fedha hizo kunatokana na usimamizi usioridhisha wa mikataba, kutofanyika kwa tathmini ya kina na upembuzi yakinifu ili kubaini uwezo halisi wa Mawakala hao kabla ya kuingia nao mikataba pamoja na kukosekana kwa uhalisia wa mapato katika vyanzo husika.

Mfano wa Halmashauri ambazo walipokea fedha pungufu ya kiasi kilichoanishwa katika mkataba na mawakala wa ukusanyaji wa

mapato ni pamoja na H/Jiji Arusha ilipokea **Sh. 1,388,859,531** ya ushuru wa taka ngumu kati ya **Sh. 9,269,635,995** iliyopo katika mikataba ya mawakala na kuacha **Sh. 7,880,776,464**. Halmashauri nyingine zilizopokea kiasi pungufu ya kiasi kilichotajwa katika mikataba ni H/W Hanang' **Sh. 4,440,193,570**, H/Jiji Mbeya **Sh. 1,021,929,648** na H/W Kaliua **Sh. Milioni 726.94**.

Mheshimiwa Spika, Mawakala wa ukusanyaji wa mapato kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji kwa mujibu wa mikataba kunaashiria upotevu wa fedha za umma na kusababisha Halmashauri husika kushindwa kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Kamati inazitaka Halmashauri zote kufanya tathmini ya kina na kufahamu uwezo halisi wa mawakala kabla ya kuingia mikataba na mawakala hao.

2.3.1.6 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutowasilisha Halmashauri Marejesho ya 20% ya Kodi ya Ardhi Sh. Bilioni 13.54

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Vifungu vya 6(1)(t) na 7(1)(y) vya Sheria ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kama vilivyorekebishwa na Vifungu vya 40 na 41 mtawalia vya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023, Halmashauri za Wilaya na Miji zinapaswa kukusanya asilimia 20 ya kodi ya pango la ardhi. Kwa muktadha huo, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambayo ndiyo inakusanya kodi ya pango la ardhi imekuwa ikichelewa kuwasilisha katika Halmashauri Asilimia 20 iliyopaswa kurejeshwa.

Kutokuwasilishwa kwa fedha hizo kunatokana na kukosekana kwa mfumo mzuri wa kudai urejeshwaji wa fedha hizo. Kwa Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati, Wizara inadaiwa jumla ya **Sh. 5,364,337,089.85**. Baadhi ya Halmashauri ambazo hazijarejeshewa Asilimia 20 ya kodi ya Ardhi zinaonekana katika **Jedwali Na 3**

Jedwali Na. 3: Halmashauri zinazoidai Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

S/N	Jina la Halmashauri	Kiasi Kisichorejeshwa
1.	H/M Kigamboni	Sh. 3,227,098,939.00
2.	H/Jiji Tanga	Sh. 587,996,317.00
3.	H/Jiji Mbeya	Sh. 412,267,944.00
4.	H/W Kilwa	Sh. 181,523,163.00
5.	H/ Mji Kasulu	Sh. 131,225,144.004

Mheshimiwa Spika, Halmashauri kushindwa kukusanya kodi ya Ardhi kutoka wizarani kunaathiri ufanisi wa utoaji wa huduma kwa jamii na kushindwa kutekelezwa kwa shughuli zilizopangwa katika mwaka husika. Halmashauri zimeileza Kamati kuhusu juhudi ambazo zimefanyika katika ufatiliaji wa madeni hayo bila ya mafanikio. Kamati inaishauri Wizara kulipa madeni yake kwa muda kwakuwa fedha hizo zimeshakusanywa.

2.3.1.7 Kutohuishwa kwa kanzi data ya walipa kodi katika Halmashauri

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zinapaswa kuwa na mfumo Madhubuti wa kukusanya, kutunza, na kuchambua taarifa zote za

watu binafsi na taasisi zinazopaswa kulipa kodi, ushuru, au ada mbalimbali ndani ya eneo la Halmashauri. Taarifa hizo zinapaswa kutunzwa katika Kanzi data ya walipakodi wa Halmashauri.

Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini upotevu wa mapato kwa baadhi ya Halmashauri uliosababishwa na kutohuishwa kwa Kanzi data ya walipa kodi wa Halmashauri hizo. Kutohuishwa kwa Kanzi data kunatokana na udhaifu wa mifumo ya udhibiti wa ndani pamoja na kukosekana usimamizi na ufuatiliaji wa Sheria na Kanuni za ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, H/Mji Babati imepoteza jumla ya **Sh. 22,235,800** kutokana na kutohuishwa kwa Leseni za biashara. Katika muktadha huo huo, H/W Tarime ilipoteza **Sh. 64,032,100** kutokana na uwepo wa biashara **765** zilizoendelea kufanya kazi kwa kutumia leseni zilizokwisha muda. Vile vile, H/M Ubungo haijahuisha leseni **13,814** zenye thamani ya **Sh.1,830,626,996**.

Mheshimiwa Spika, Kutohuishwa kwa Kanzi data ya walipa kodi kunaashiria upotevu wa fedha za umma ambazo zingeweza kutekeleza majukumu mengine kwa maslahi mapana ya wananchi. Kamati imekuwa ikizielekeza Halmashauri zote kuhakikisha zinakuwa na taarifa sahihi za walipa kodi wote waliopo katika maeneo yao ya usimamizi.

2.3.1.8 Upotevu wa Mapato unaotokana na Mashauri kuwa TAKUKURU kwa muda Mrefu

Mheshimiwa Spika, Tarehe 29 Oktoba, 2024, Bunge liliazimia kwa kuitaka Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi za RAS katika mikoa yote kufuatilia na kubainisha mashauri yote yaliyopo TAKUKURU yanayohusishwa na fedha zilizokusanywa katika Halmashauri. Lengo la Azimio hilo lilikuwa ni kuitaka Mamlaka hiyo kuharakisha mchakato wa uchunguzi ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zimekuwa zikiieleza Kamati kuwa, zimekuwa zikishindwa kuchukua hatua kwa haraka kwa kuwa, mashauri mengi ya upotevu wa fedha za Umma bado yapo TAKUKURU kwa muda mrefu kwa ajili ya uchunguzi. Aidha, Kamati imebaini pia uwepo wa kesi ambazo, kimsingi zilipaswa kuwa ni mashauri ya kipolisi na badala yake yamewasilishwa TAKUKURU. Hali hii inachelewesha uchukuaji wa hatua stahiki ambazo zingesaidia kuzuia upotevu wa fedha za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo sasa, Halmashauri zimekuwa zikiitumia TAKUKURU kama sehemu ya kuchelewesha kufanyika kwa maamuzi hasa kwa mashauri ambayo tayari yana Ushahidi badala ya kuwasilisha kesi hizo polisi. Mfano wa Halmashauri ambazo zimebainika kuwa na changamoto hii ni H/W Kasulu na H/W Nachingwea.

Mheshimiwa Spika, H/W kasulu ilipeleka TAKUKURU suala la matumizi yenye shaka yaliyosababisha upotevu wa **Sh. 146,178,000.00**. Mapitio ya taarifa za benki yalibaini kuwa, kiasi hicho cha fedha kilitolewa na Mhasibu wa Halmashauri toka katika akaunti za benki za vituo Nane vya afya na kutumika bila kuwa na idhini na vielelezo vya uthibitisho. Kiasi hicho hakikuoneshwa katika vitabu husika vya fedha vya vituo hivyo vya afya.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa waliohusika na upotevu huu wa fedha wako chini ya Mamlaka ya Afisa Masuuli na ushahidi upo bayana hivyo walitakiwa kuchukuliwa hatua za kisheria kwa kupeleka kesi Polisi badala TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, katika hoja kama hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea ililipa **Sh. 123,048,000** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi tarehe 12 Januari, 2025. Hata hivyo, hakukuwa na vielelezo vinavyothibitisha kuwa vifaa hivyo vilipokelewa, kukaguliwa au kurekodiwa kwenye rejista ya stoo. Hadi kufikia Oktoba, 2025 vifaa hivyo vilikuwa havijapokelewa, hivyo Halmashauri ikapeleka suala hili TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa suala hili linahusu usimamizi wa mkataba (manunuzi ya vifaa) hivyo Halmashauri ilitakiwa kupeleka polisi ili liweze kushughulikiwa kwa haraka.

2.3.2 Matumizi ya Fedha za Umma kinyume na Sheria na Kanuni pamoja na usimamizi usioridhisha wa Akaunti ya Amana

Mheshimiwa Spika, jukumu kuu la Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa ni kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika Taarifa ya CAG. Jukumu hilo lipo kwa mujibu wa Kifungu cha 14 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

Katika kuhakikisha kunakuwa na mnyororo thabiti wa uwajibikaji katika matumizi ya fedha za Serikali za Mitaa, Kamati imekuwa ikijiridhisha iwapo matumizi ya kila Halmashauri yanazingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali. Vile vile, Kamati imefanya uchambuzi wa matumizi ya fedha za Mfuko wa Amana ili kujiridhisha iwapo fedha hizo zinatumika kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa Ripoti ya CAG kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Mwezi Juni, 2025, Kamati imebaini changamoto kadhaa katika matumizi ya fedha za Umma kama ifuatavyo: -

2.3.2.1 Matumizi yasiyo sahihi ya Fedha za Bakaa

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 21 ya kanuni za Bajeti za Mwaka 2015 inaeleza kuhusu fedha za Bakaa (carry-over funds) na matumizi ya fedha ambazo hazikutumika ndani ya mwaka wa fedha husika. Pamoja na Sheria na Kanuni kuruhusu matumizi ya fedha za bakaa, Kanuni ya 21(3) ya Kanuni za Bajeti za Mwaka 2015 imefafanua juu

ya urejeshwaji wa fedha hizo katika Mfuko Mkuu wa Serikali iwapo hazitatumika. Uwepo wa Kanuni hizi unalenga kuhakikisha fedha ambazo hazikutumika kwa wakati zinadhibitiwa na kuhamishwa kwa utaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati, imebainika uwepo wa Halmashauri zenye fedha za bakaa ambazo hazijatumika ndani ya muda unaotakiwa pamoja na kutumia fedha hizo katika miradi ambayo haikukusudiwa. Kushindwa kutumika kwa fedha hizo ndani ya muda uliopangwa kunatokana na Halmashauri kuchelewa kufanya usuluhishi wa shughuli zilizopangwa kufanyika.

Fedha za bakaa kutotumika ndani ya muda uliopangwa na kwa miradi iliyokusudiwa kunaongeza uwezekano wa matumizi mabaya ya fedha za Halmashauri na wananchi wanakosa huduma ambazo zingepatikana kutokana na kutekelezwa kwa miradi mbalimbali. Mfano wa Halmashauri ambazo zilishindwa kutumia fedha za bakaa ni pamoja na H/W Mbozi **Sh. 1,068,556,526** (ambapo **Sh. 1,018,556,526** ni kwa ajili ya ujenzi wa shule ya wavulana Songwe na **Sh. 50,000,000** ya ununuzi wa Generator). Vile vile, H/ Jiji Dodoma imeshindwa kutumia **Sh. 2,423,375,329** ndani ya muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikifanya uchambuzi wa kina wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za bakaa. Taarifa zinazoangaliwa zinajumuisha salio anzia, fedha zilizopokelewa, matumizi katika mwaka husika, utekelezaji wa miradi na salio ishia.

Uchambuzi wa taarifa hizo huisaidia Kamati kubaini iwapo Sheria na Kanuni za matumizi ya fedha za bakaa zimezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Wakati wa mahojiano na Maafisa Masuuli, imebainika baadhi yao kutokuwa na matumizi sahihi ya fedha za bakaa na kushindwa kutoa mchanganuo sahihi wa namna fedha hizo zilivyotumika. Kamati inasisitiza matumizi sahihi ya fedha za bakaa ili kukidhi matakwa ya Sheria na Kanuni.

2.3.2.2 Kuchelewa kurejeshwa kwa Masurufu ndani ya muda ulioidhinishwa Sh. 1,016,728,241

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka utaratibu wa utoaji wa masurufu kwa watumishi wa umma kwa ajili ya safari ya kikazi, semina au mafunzo, kufanya ukaguzi na ufuatiliaji na shughuli nyingine rasmi zilizoidhinishwa. Utoaji, utumiaji na urejeshaji wa masurufu umewekewa utaratibu katika Sheria ya fedha za Serikali za Mitaa Sura 290, Sheria ya Fedha za Umma na Kanuni zake pamoja na Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa.

Agizo namba 40(3) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linataka masurufu maalum yarejeshwe ndani ya wiki mbili baada ya kukamilika kwa shughuli husika na endapo hayatarejeshwa yakatwe katika mshahara wa mtumishi. Vile vile, Agizo namba 40(4) inazuia Halmashauri kutoa masurufu mengine kabla ya masurufu ya awali kurejeshwa.

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya CAG imebainisha uwepo wa baadhi ya watumishi wa Halmashauri kutorejesha masurufu kwa muda uliopangwa na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na Maafisa Masuuli. Uwepo wa hoja hiyo unasababishwa na Halmashauri kutokuwa na mifumo madhubuti ya udhibiti wa mifumo ya ndani pamoja na kutokuwa na ufuatiliaji uliojitosheleza. Mfano wa Halmashauri zenye madeni ya masurufu ni H/W Mlele **Sh. 33,941,000**, H/Jiji Mbeya **Sh. 21,080,000.00** na H/W Mbeya **Sh. 22,340,103.22**.

Mheshimiwa Spika, Watumishi kutorejesha masurufu kwa wakati na hatua stahiki kutochukuliwa na Maafisa Masuuli kunadhoofisha uwajibikaji wa kifedha na kuongeza hatari ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kamati imekuwa ikiwakumbusha Maafisa Masuuli kutekeleza wajibu wao kwa kuhakikisha hatua stahiki zinachukuliwa.

2.3.2.3 Matumizi ya Fedha za Mfuko wa Amana kinyume na Sheria, Kanuni na Miongozo

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya fedha za amana (deposit funds) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa huongozwa na Kanuni na Miongozo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001, Kanuni za Bajeti za mwaka 2015, Mwongozo wa mfumo wa malipo ya kielektroniki ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa uliotolewa na OWM-TAMISEMI mnamo Mwezi Septemba 2017, na Mwongozo wa utawala wa mapato ya Mamlaka za Serikali za

Mitaa wa mwaka 2019. Miongozo hiyo imewekwa ili kuzuia matumizi yasiyo halali na yasiyothibishwa ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Kifungu cha 14 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025 inatekelezwa kikamilifu, Kamati imebaini uwepo wa baadhi ya Halmashauri kutumia fedha za Mfuko wa amana kinyume na Kanuni na Miongozo iliyowekwa. Miongoni mwa ukiukwaji uliofanywa na baadhi ya Halmashauri ni pamoja na matumizi ya fedha za amana zaidi ya kiwango kilichowekwa, uhamishaji wa fedha bila idhini na kuazima fedha za Mfuko wa Amana bila kurejesha.

Baadhi ya Halmashauri zilizohojiwa na Kamati ambazo hazikuzingatia matumizi sahihi ya fedha za Mfuko wa Amana ni H/W Bunda ambayo ilitumia fedha za amana zaidi ya kiasi kilichowekwa kwa **Sh. 287,229,060**, kinyume na Kanuni ya 132 ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001. Vile vile, H/M Shinyanga ilitumia jumla ya **Sh. 104,926,312** kutoka katika Akaunti ya Amana kwa ajili ya kufadhili shughuli za kawaida kinyume na Kanuni ya 115 ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001.

Mheshimiwa Spika, Sababu za ukiukwaji wa Kanuni na Miongozo iliyotajwa ni kukosekana kwa udhibiti wa akaunti ya Amana. Kamati inaendelea kuzisisitiza Halmashauri zote kuzingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na Miongozo katika utendaji wa kazi wa kila siku ili kuimarisha ustawi wa wananchi.

2.3.2.4 Matumizi zaidi ya Bajeti iliyotengwa kwa Ajili ya Klabu za Michezo Zinazomilikiwa na Halmashauri Sh. Bilioni 2.13.

Mheshimiwa Spika, Sheria za Serikali za Mitaa zinaipa mamlaka kila Halmashauri kukuza ustawi wa kijamii, kiuchumi, burudani, na afya ya wakazi wake. Michezo (ikiwemo mpira wa miguu) inatafsiriwa kama sehemu ya maendeleo ya kijamii, ustawi, na burudani kwa jamii husika. Kwa muktadha huo, Halmashauri mbalimbali nchini ziliweza kuanzisha au kununua na kumiliki klabu za mpira wa miguu ambazo zinashiriki Ligi Kuu ya Tanzania Bara na madaraja mengine.

Aya ya 21.9(b) ya Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2019 inamtaka Mweka Hazina kuhakikisha matumizi hayazidi bajeti. Hata hivyo H/jiji la Mwanza na H/Jiji la Dodoma zilifanya matumizi zaidi ya bajeti iliyotengwa kwa timu za Pamba Jiji FC na Dodoma Jiji FC mtawalia.

Mheshimiwa Spika, H/Jiji Mwanza ilitumia **Sh. Bil 1.48** kwa timu ya Pamba Jiji, matumizi ambayo hayakuwa kwenye bajeti ya mwaka iliyoidhinishwa. Vile vile, H/Jiji Dodoma ilipanga bajeti ya **Sh. Mil 745** kwa ajili ya Dodoma Jiji FC lakini ilitumia **Sh. Bil 1.17**, na hivyo kuzidisha kiasi cha **Sh. Mil 427.70** kinyume na Sheria, Kanuni na Miongozo.

Mheshimiwa Spika, Matumizi zaidi ya bajeti iliyopangwa yanatokana na mifumo dhaifu ya ufuatiliaji wa matumizi ya Halmashauri. Uchepushaji wa fedha hizo unachochea matumizi yasiyo sahihi ya fedha za umma na kusababisha matumizi yaliyopangwa

awali kutofanyika. Ushauri wa Kamati kwa Halmashauri ni kuhakikisha Maafisa Masuuli wanaimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa matumizi yote ya Halmashauri.

2.3.3 Ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na mapungufu katika usimamizi wa Mikataba

Mheshimiwa Spika, wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, Kamati imepitia maeneo muhimu ya ununuzi wa umma kama upangaji wa ununuzi, uzingatiaji wa taratibu za zabuni, na usimamizi wa mikataba. Uchambuzi wa Kamati katika maeneo hayo umeongozwa na Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023 na Kanuni za ununuzi wa umma za mwaka 2024.

Maeneo yaliyobainika kutokuwa na uzingatiaji wa Sheria ya ununuzi wa umma ni kama yafuatayo:-

2.3.3.1 Halmashauri Kufanya Ununuzi wa Shilingi Bilioni 9.90 nje ya mfumo wa ununuzi wa kielekitroniki (NeST)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mfumo wa ununuzi wa kielektroniki (NeST) kwa lengo la kuongeza uwazi na ushindani, kupunguza gharama na muda, kuzuia kughushi na udanganyifu, kuboresha uwajibikaji na kurahisisha upatikanaji wa taarifa, na kusimamia shughuli zote za manunuzi na zabuni za umma kwa njia ya mtandao.

Katika Mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2025 Halmashauri 59 zilifanya ununuzi nje ya mfumo wa ununuzi wa kielektroniki

wenye jumla ya **Sh. 9,900,179,127** kinyume na Kifungu cha 73(1) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023. Licha ya kuwa hoja hii imepungua kutoka **Sh. Bil 31.81** iliyoripotiwa katika mwaka wa fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2024, Kamati inaendelea kuzisisitiza Halmashauri zote kutumia mfumo huo wa kielektroniki.

Wakati wa majadiliano na Maafisa Masuuli, Halmashauri zilizofanya ununuzi nje ya mfumo wa NeST ni H/W Tarime **Sh. 252,958,432**, H/W Geita **Sh. 113,896,500** na H/M Musoma **Sh. 159,118,088**.

Mheshimiwa Spika, ununuzi kufanyika nje ya mfumo kunaondoa dhamira njema ya Serikali ya kuhakikisha Halmashauri zote zinaboresha uwajibikaji na kutoa fursa kwa wananchi wenye dhamira ya kufanya biashara na Halmashauri kupata nafasi hiyo. Aidha Kamati inasisitiza Halmashauri kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 73 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura ya 410, Kanuni ya 11 ya Kanuni za ununuzi wa Umma 2024 na Waraka wa Hazina Na. 2 wa 2023/24.

2.3.3.2 Ununuzi Usiotumia Njia za Ushindani (Restricted Tendering)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zote zinapaswa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma katika upangaji wa ununuzi ili kukuza upatikanaji wa bidhaa na huduma kwa njia ya ushindani na kutoa muda wa kutosha kwa ajili ya tathmini ya soko na kuthibitisha njia sahihi za ununuzi zinazotumiwa. Ili Kukidhi matakwa ya Sheria, Halmashauri hutumia zabuni ya wazi (Open Tendering) ambapo mtu yeyote mwenye sifa anaweza kuomba.

Kanuni ya 152(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2024 inaruhusu matumizi ya ununuzi usiotumia njia ya ushindani (Restricted Tendering) ambayo, fursa ya kuomba zabuni haitolewi kwa umma wote, bali hualikwa wazabuni maalum tu waliochaguliwa na taasisi inayohitaji huduma au bidhaa.

Mheshimiwa Spika, Kanuni imeruhusu matumizi ya njia hii iwapo kuna dharula au uharaka wa muda, bidhaa, kazi au huduma inahitaji utaalamu maalumu. Kinyume na Kanuni zilizopo, baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikitumia njia zisizo za ushindani katika Ununuzi bila ya kuwepo kwa sababu zilizotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2024, H/Mji Njombe ilitumia njia isiyo ya ushindani kinyume na Kanuni ya 163 na 164 za Kanuni za Ununuzi wa Umma 2024 kumpata Mkandarasi Ms. GF Truck Limited kwa Mkataba Na. 73D7/2024/2025/G/195 kwa ajili ya ununuzi wa gari la maji taka kwa gharama ya **Sh. 326,363,399**. Gari hilo lilipaswa kuwasilishwa ndani ya **siku 90** baada ya mkataba kusainiwa.

Kinyume na matakwa ya mkataba huo, Tarehe 23/10/2024 Halmashauri ilifanya malipo kwa mzabuni kabla ya gari kupokelewa. Aidha, Halmashauri haikumtoza mzabuni fidia ya ucheleweshaji licha ya mzabuni kukaa na fedha za umma kwa muda wa **miezi Tisa** bila ya kuwasilisha gari hilo. Pamoja mapungufu hayo, Halmashauri ilifanya malipo ya awali bila ya kupata dhamana ya malipo hayo.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 16/03/2026 gari liliwasilishwa na kupokelewa na Halmashauri. Hata hivyo halikukidhi viwango vilivyotajwa katika mkataba wa manunuzi hivyo gari inabidi lirudishwe kwa mzabuni. Mpaka kipindi ambacho Halmashauri ilikutana na Kamati, Gari hilo limetelekezwa na mzabuni katika maegesho ya viwanja vya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Mfano mwingine wa Halmashauri zilizotumia njia isiyo ya ushindani bila ya kuwa na ushahidi wa kutosha unaothibitisha mazingira yaliyohalalisha matumizi ya njia hiyo ni H/W Bukombe iliyotoa mikataba 13 yenye thamani ya **Sh. 19,943,396,910**, H/W Geita iliyotumia **Sh. 665,001,100** katika mikataba Sita na H/W Kishapu **Sh. 27,550,000**.

Mheshimiwa Spika, kutozingatiwa kwa Kanuni tajwa hapo juu kunaongeza hatari ya kupata bidhaa na huduma zisizo na ubora, kupunguza uwazi, na kupata bei zisizo na ushindani. Ni matumaini ya Kamati kuwa, Halmashauri zote zitazingatia matakwa ya Kanuni hiyo ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika Ununuzi wa Umma.

2.3.3.3 Mapungufu katika Tathimini ya Zabuni

Mheshimiwa Spika, mchakato wa tathimini ya zabuni katika Mamlaka za Serikali za Mitaa unatakiwa kuzingatia Kifungu cha 55(1) cha Sheria ya Ununuzi ya Umma ya Mwaka 2023. Kinyume na matakwa ya kifungu hicho, baadhi ya Halmashauri iliwaondoa bila sababu za msingi wazabuni waliotoa bei ya chini zaidi iliyofanyiwa tathmini, wenye zabuni za jumla ya **Sh. Bilioni 28.70**.

Kamati imebaini kuwa, kuondolewa kwa wazabuni waliotoa bei ya chini zaidi bila sababu za msingi kumetokana na kutokuwepo kwa mifumo thabiti ya uzingatiaji wa Sheria katika baadhi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, H/W Kaliua haikuzingatia matakwa ya kanuni ya 16(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2024 na kusababisha ongezeko la gharama la **Sh. milioni 684.4** linalotokana na Ununuzi wa mtambo wa kutengeneza barabara (motor grader). Halmashauri ilinunua mtambo kutoka kampuni ya OREMET International (T) Limited kwa **Sh 1,227,200,000** (pamoja na VAT). Ongezeko hilo lilisababishwa na kukataliwa kwa zabuni ya bei ya chini ya **Sh 542,800,000** (pamoja na kodi ya VAT) kutoka kampuni ya GF Trucks & Equipment Limited.

Mheshimiwa Spika, Mapungufu kama hayo ya tathimini ya zabuni yamebainika pia katika H/W Bukombe ambapo Halmashauri ilitoa tuzo ya zabuni sita zenye thamani ya **Sh. 19,629,448,436** ambazo zilitathminiwa kwa kutumia vigezo ambavyo havikuwa wazi. Vile vile, H/M Shinyanga ilitoa tuzo ya zabuni kwa mzabuni mwenye bei kubwa na kusababisha Halmashauri kupata Hasara ya **Sh. 622,727,000**.

CAG aliieleza Kamati kuwa, zabuni hizo zilitolewa kwa wazabuni wa chini kabisa kwa kutumia vigezo ambavyo havikuwekwa bayana kwenye nyaraka za zabuni kama vile tathmini ya uwezo wa kifedha na utoshelevu wa vifaa muhimu.

Mheshimiwa Spika, kutozingatiwa kwa taratibu kunasababishwa na kutokufuatwa kwa taratibu za tathimini, kutokuwa na timu ya tathmini yenye watu wenye uzoefu wa kutosha na wenye uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi na kukosekana kwa umakini wakati wa tathmini. Aidha, tathmini zenye kasoro zinaongeza hatari ya upotevu wa fedha za Umma, uwezekano wa migogoro ya kimkataba, na kupunguza imani ya umma katika mfumo wa ununuzi.

Kamati inazishauri Halmashauri zote nchi kuhakikisha zinafanya tathmini ya kina ya uwezo wa kisheria, kiufundi, na kifedha wa wazabuni wote.

2.3.3.4 Mapungufu katika usimamizi wa Mikataba

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kunakuwa na usimamizi Madhubuti wa mikataba katika nyanja zote, Kamati imeangazia maeneo mbalimbali kama mikataba kusainiwa ndani ya muda ulioainishwa na Kanuni, Mikataba kusainiwa bila kupekuliwa na Mwanasheria, Mikataba kutolewa zaidi ya gharama za Mhandisi na Malipo kwa wakandarasi kinyume na Kanuni,

Mheshimiwa Spika, katika eneo la uzingatiaji wa muda wa kusaini mikataba baada ya mchakato wa zabuni kukamilika, Kanuni ya 240(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2024 imeweka sharti kwa Taasisi ya ununuzi.

Uchambuzi wa Kamati katika eneo hili ulibaini uwepo wa Halmashauri ambazo zilichelewesha zoezi la kusaini mikataba tofauti na matakwa ya Kanuni zilizowekwa. Changamoto kama hii ilibainika katika H/W

Bukombe ambapo, mikataba minne yenye thamani ya jumla ya **Sh. 22,737,107,520.92** ilichelewa kusainiwa kwa kati ya siku 34 na 48 tangu kutolewa kwa taarifa za tuzo za zabuni.

Mheshimiwa Spika, Mikataba kutosainiwa kwa wakati kumesababishwa na uzingatiaji hafifu wa Sheria na kanuni. Maafisa Masuuli walikiri ucheleweshaji huo na kuieleza Kamati kuwa, wataongeza ufuatiliaji wa hatua za manunuzi ili mikataba ijayo iandaliwe, iidhinishwe na kusainiwa ndani ya muda uliowekwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine katika usimamizi wa mikataba ni mikataba kusainiwa bila kupekuliwa na Mwanasheria. Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Sura ya 268) inaipa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mamlaka ya kuratibu, kuandaa, na kufanya upekuzi (vetting) wa mikataba yote inayohusisha taasisi za umma, zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Vile vile, Kanuni ya 59 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 (kama zilivyorekebishwa mwaka 2016 na 2025) imeweka ukomo wa kiasi cha thamani ya mkataba inayopaswa kupekuliwa na kupitishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na ile inayopaswa kupitiwa na Mwanasheria wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelekezo yaliyoainishwa katika Sheria na Kanuni hizo, H/W Tarime ilisaini jumla ya mikataba 18 yenye thamani ya **Sh. 586,611,473.04**, H/W Bunda ilisaini

mikataba 40 yenye jumla ya **Sh. 1,236,496,534** na H/W Iringa ilisaini mikataba ya **Sh. 674,302,350** bila ya kupekuliwa na Mwanasheria wa Halmashauri.

Kamati imebaini kuwa, kutosainiwa kwa mikataba hiyo kunasababishwa na kutokuwepo kwa mazingatio ya Sheria na Athari yake ni kuziweka Halmashauri hizo katika hatari ya kuingia katika mikataba isiyo na tija.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lenye mapungufu katika usimamizi wa mikataba ni Mikataba kutolewa zaidi ya gharama za Mhandisi ambapo, Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake imekataza utoaji wa mikataba inayozidi makadirio ya Mhandisi (Engineer's Estimate). Taarifa ya CAG kwa mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2025 imebainisha baadhi ya Halmashauri kutoa tuzo ya mkataba ambayo thamani yake inazidi bajeti iliyotengwa au makadirio ya gharama halisi za soko zilizoidhinishwa.

Halmashauri hizo ni pamoja na H/W Bukombe ambayo ilisaini mikataba miwili yenye thamani ya **Sh. 21,890,849,280.92** ambapo makadirio ya Mhandisi yalikuwa ni **Sh. 20,960,735,216.56** na hivyo kuzidi makadirio kwa **Sh. 930,114,064.36** bila ya kuwa na ushahidi wa kuthibitisha kuwa idhini ya awali ya gharama za ziada ilipatikana kutoka mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, mapungufu katika usimamizi wa mikataba pia yameonekana pia katika malipo yaliyofanywa kwa wakandarasi kinyume na Kanuni. Kamati ilifanya mahojiano na H/Jiji Dodoma na

kubaini kufanyika kwa malipo ya awali yenye thamani ya **Sh. 399,319,900** kwa mkandarasi aliyezuiliwa kufanya kazi.

Halmashauri iliingia Mkataba Na. 7205/2024/2025/W/25 wa kampuni ya Gopa Construction Tanzania Limited tarehe 20 Mei 2025 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la shule ya sekondari ya ghorofa katika kata ya Chahwa kwa thamani ya **Sh. Bilioni 3.99**.

Mapitio ya utekelezaji wa mkataba huo yamebaini kuwa, mkandarasi huyo alikuwa amefungiwa kushiriki zabuni (debarment) na Mamlaka ya Ununuzi wa umma (Public Procurement Regulatory Authority), ambapo zuio hilo lilianza kutumika tarehe 20 Mei 2025 hadi 19 Mei 2026. Halmashauri kuendelea kumtumia mkandarasi huyo kulitokana na kutofanyika kwa uhakiki wa hali ya mkandarasi kabla ya kusaini mkataba na kutothibitishwa kwa uhalali wa dhamana husika na benki iliyozitoa kabla ya kufanya malipo ya awali.

Mheshimiwa Spika, Hadi Kamati ilipokutana na Halmashauri Mwezi Juni, 2026 utekelezaji wa mradi huu ulikuwa umesimama tangu mwezi Aprili 2026 na hapakuwa na mabadiliko kulinganisha na ukaguzi wa awali. Kamati inawashauri Maafisa Masuuli kuimarisha usimamizi wa mikataba ili kuongeza tija ya utekelezaji wa miradi kwa maslahi mapana ya taifa.

2.3.3.5 Mabadiliko ya gharama za Mkataba bila ya kupata Kibali cha Mamlaka

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 316(1) na (3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 inayohusu mabadiliko ya mkataba

(contract variations) inazitaka Halmashauri kupata idhini kutoka kwa Mamlaka husika yenye dhamana ya kuidhinisha bajeti (Paymaster General). Licha ya matakwa ya Kanuni hiyo, Kamati imebaini uwepo wa Halmashauri ambazo zilifanya mabadiliko ya gharama za Mkataba bila ya kupata idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Baada ya uchambuzi wa kina wa Ripoti ya CAG, H/Jiji Mwanza imebainika kufanya mabadiliko ya Mkataba Na. 8118/2023/2024/W/01 kati ya Halmashauri ya Jiji na Mkandarasi M/s Comfix and Engineering Ltd unaohusu ujenzi wa Soko la Samaki Mkuyuni. Mkataba huo wenye thamani ya awali ya mkataba ya **Sh. 7,364,387,337.50** ulipangwa kuanza 14/11/2024 hadi 14/11/2025. Baada ya mapitio ya usanifu, gharama mpya za mkataba zilifikia **Sh. 20,887,641,200.91** sawa na ongezeko la **Asilimia 183.6** la gharama za awali za Mkataba.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya mkataba yaliyofanyika yamesababisha ongezeko la **Bilioni 13.52**. Aidha, Kutokana na mabadiliko ya gharama na wigo wa mradi, mradi huu haujaanza kutekelezwa licha ya kufanyika kwa malipo ya awali kwa mkandarasi ya **Sh.1,104,658,100.63**.

Ili kuondoa changamoto hii, Kamati inazitaka Halmashauri zote kuhakikisha kuwa, mabadiliko ya wigo wa mradi yanaainishwa na kuthibitishwa. Aidha, mabadiliko ya gharama za mradi yaidhinishwe na mamlaka husika yenye dhamana ya kuidhinisha bajeti au Mlipaji Mkuu wa Serikali kabla ya utekelezaji wake.

2.3.3.6 Mapungufu ya Kimkataba katika Upangishaji wa Hoteli ya Dodoma Jiji

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 21 (1) cha Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi (Public Private Partnership Act – PPP) kinazitaka Taasisi za Umma kulinda maslahi ya umma. Kinyume na Kifungu hicho, Halmashauri iliingia Mkataba Na. LGA/20/2021-2022/NCS/09 kwa ajili ya upangishaji wa Dodoma City Hotel kwa kipindi cha miaka 10.

Mapungufu yaliyobainika katika Mkataba huo ni mfumo wa upangishaji uliotumika wenye udhaifu ambao unategemea kodi ya pango isiyobadilika, kiwango cha urejeshaji wa uwekezaji (Return on Investment) kuwa ni **Asilimia 7.99** pekee badala ya **Asilimia 20.15** iliyokadiriwa. Udhaifu katika mfumo wa upangishaji umesababisha muda wa kurejesha mtaji kuongezeka kutoka **miaka 5** hadi **miaka 19**.

Mheshimiwa Spika, mapungufu mengine katika Mkataba huo wa upangishaji ni pamoja na dhamana ya utekelezaji wa mkataba kumalizika kwa muda wake tangu Tarehe 31 Mei, 2024 bila ya kuhuishwa, Mkataba kutokuwa na sharti la kumtaka mpangaji kuwasilisha taarifa za fedha za Hoteli kwa Halmashauri, na Mkataba kutokuwa na masharti yanayoweka adhabu au riba kwa malipo ya kodi ya pango yanayocheleweshwa.

Athari za Halmashauri kushindwa kusimamia mkataba ipasavyo kulisababisha Hasara ya **Sh. 21,144,412** ambayo ililipwa kwa ajili ya gharama za bima ambazo zilipaswa kulipwa na mpangaji. Vile vile, mradi umekuwa na utendaji duni wa kifedha uliopelekea Halmashauri kukosa mapato yaliyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeelezwa na Halmashauri kuwa, kuanzia mwaka wa 10 wa Mkataba, marekebisho ya kodi ya pango yatazingatia utendaji halisi wa biashara ili kufupisha muda wa urejeshaji. Kamati inaishauri Halmashauri kuondoa dosari za kimkataba wakati wa mapitio ili Mkataba huo uweze kuleta tija.

2.3.4 Madeni ya Halmashauri kutolipwa kwa wakati (Payables)

Mheshimiwa Spika, Uwepo wa madeni katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni moja ya changamoto zinazogusa usimamizi wa fedha za umma katika uendeshaji wa Halmashauri, na utoaji wa huduma kwa wananchi. Madeni ya Halmashauri yanajumuisha madeni ya watumishi, madeni ya wazabuni na madeni mengineyo ambayo yanapaswa kulipwa na Serikali Kuu pamoja na Halmashauri husika kupitia mapato yake ya ndani. Uchambuzi wa Kamati umeangalia maeneo yafuatayo: -

2.3.4.1 Madeni ya Watumishi

Mheshimiwa Spika, kwa Halmashauri 75 ambazo taarifa zake zimechambuliwa na Kamati, watumishi walikuwa wanazidai Halmashauri zao jumla ya **Sh. 53,352,423,426.32** (Madeni ya

Serikali Kuu na Madeni ya Halmashauri). Uwepo wa madai mengi unatokana na kuchelewa kuwasilishwa na kuhakikiwa kwa madeni hayo, upungufu wa mapato ya ndani, kuchelewa kwa ruzuku ya Serikali pamoja na kutozingatiwa kwa umri wa madeni wakati wa malipo.

Kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2025, jumla ya **Sh. 34,071,848,019.52** ni madeni ya watumishi ya muda mrefu yanayopaswa kulipwa na Serikali Kuu. Baadhi ya madeni hayo yameoneshwa katika Jedwali **Namba 4** ya Taarifa Hii.

Jedwali Na. 4: Madeni ya Watumishi yanayopaswa kulipwa na Serikali Kuu zaidi ya Bilioni moja

S/N	Jina la Hamashauri	Kiasi
1.	H/W Bahi	Sh. 2,441,290,461.00
2.	H/W Masasi	Sh. 1,985,865,399.00
3.	H/Jiji Dodoma	Sh. 1,892,244,668.49
4.	H/W Meru	Sh. 1,363,588,194.00
5.	H/Jiji Mwanza	Sh. 1,301,705,057.00
6.	H/W Ukerewe	Sh. 1,203,381,085.00
7.	H/M Kigoma	Sh. 1,110,363,855.00
8.	H/W Buhigwe	Sh. 1,072,223,748.00
9.	H/W Sengerema	Sh. 1,000,198,212.00

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madai ya watumishi ambayo yanapaswa kulipwa na Halmashauri husika, Jumla ya **Sh. 19,280,575,406.80** kutoka katika Halmashauri 75 hazikulipwa

kwa wakati. Orodha ya Halmashauri zinazodaiwa zaidi ya Sh. Bilioni Moja na kiasi cha madeni hayo imeoneshwa katika Jedwali Namba 5.

Jedwali Na. 5: Madeni ya Watumishi yanayopaswa kulipwa na Halmashauri zaidi ya Bilioni Moja

S/N	Jina la Hamashauri	Kiasi
1.	H/W Iringa	Sh. 1,527,646,280.00
2.	H/W Gairo	Sh. 1,454,897,893.00
3.	H/Mji Sumbawanga	Sh. 1,352,121,312.00
4.	H/W Njombe	Sh. 1,290,133,891.00
5.	H/W Rungwe	Sh. 1,168,825,158.00
6.	H/W Bariadi	Sh. 1,002,140,041.88

Mheshimiwa Spika, maelezo yaliyotolewa na Maafisa Masuuli juu ya kutowalipa watumishi kwa muda mrefu hayakuwa ni yenye kuridhisha kwakuwa, hapakuonekana nia thabiti ya kulipa madeni hayo kwa wakati. Vile vile, Kamati imebaini Halmashauri nyingi kutotenga bajeti ya kutosha ya ulipaji wa madeni yake. Mfano wa Halmashauri ambazo hazikutenga bajeti ya kutosha ya ulipaji wa madeni ni Jedwali namba 6.

Jedwali Na. 6: Halmashauri zilizotenga bajeti pungufu ya ulipaji wa madeni

S/N	Jina la Hamashauri	Deni Lililopo	Bajeti Iliyotengwa
1.	H/W Bagamoyo	Sh. 1,718,970,475.00	Sh. 149,379,540.00
2.	H/Mji Kasulu	Sh. 1,335,888,984.00	Sh. 195,910,473.00

S/N	Jina la Hamashauri	Deni Lililopo	Bajeti Iliyotengwa
3.	H/W Kibaha	Sh. 2,085,758,966.00	Sh. 413,946,000.00
4.	H/M Kibaha	Sh. 1,795,450,287.00	Sh. 450,000,000.00
5.	H/W Muheza	Sh. 1,931,404,594.00	Sh. 50,000,000.00
6.	H/W Namtumbo	Sh. 1,721,512,673.00	Sh. 107,350,000.00
7.	H/M Sumbawanga	Sh. 4,130,942,424.00	Sh. 302,680,000.00
8.	H/W Busega	Sh. 1,676,620,673.00	Sh. 150,000,000.00
9.	H/Mji Makambako	Sh. 1,245,038,294.00	Sh. 159,840,112.00
10.	H/Mji Njombe	Sh. 1,493,520,517.00	Sh. 239,239,331.00

Mheshimiwa Spika, Wakati wa kupitia rejista ya madeni ya kila Halmashauri, Kamati ilibaini uwepo wa madeni ya muda mrefu hadi kufikia umri wa miaka mitano yanayohusiana na posho za uhamisho, likizo, au malipo ya saa za ziada. Aidha, Watumishi wengi walioathirika ni kutoka Idara ya Elimu na Idara ya Afya.

Kutolipwa kwa madeni ya watumishi kwa muda mrefu kunasababisha kushuka kwa tija, ufanisi na morali ya kazi hali inayoathiri ubora wa huduma wanayoitoa kwa jamii, kuongezeka kwa vitendo vya ubadhilifu na kupoteza imani na mwajiri hali inayojenga hisia za kutothaminiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeelezwa kuwa, Serikali (Hazina na Halmashauri) inaendelea na ulipaji wa madeni hayo kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, kasi ya ulipaji wa madeni hayo haiendani na umri na ukubwa wa madeni yaliyopo. Kamati inaishauri

Serikali kuwa na mkakati madhubuti wa ulipaji wa madeni ya muda mrefu ili kuimarisha ustawi wa watumishi wake.

2.3.4.2 Madeni ya Wazabuni

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imefanya uchambuzi wa madeni ya wazabuni (watoa huduma) yanayopaswa kulipwa na Serikali kuu (Hazina na Halmashauri) kwa mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2025. Kwa Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati, kuna madeni ya wazabuni yenye jumla ya **Sh. 65,252,269,411.77**.

Uwepo wa madeni ya wazabuni katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kunatokana na kutotekelezwa kwa matakwa ya mikataba, kuchelewa kwa fedha za utekelezaji wa miradi, kutotoa kipaumbele katika ulipaji wa madeni pamoja na upungufu wa mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kazi cha mwezi Agosti na Oktoba, Kamati imebaini uwepo wa madeni yenye jumla ya **Sh. 8,748,199,317.15** ambayo yanapaswa kulipwa na Serikali Kuu. Orodha ya baadhi ya Halmashauri zenye madeni makubwa ni kama inavyoonekana kwenye jedwali namba 7.

Jedwali Na. 7: Madeni ya Wazabuni yanayopaswa kulipwa na Serikali Kuu zaidi ya Milioni Mia Tano

S/N	Jina la Hamashauri	Kiasi
1.	H/M Tabora	Sh. 1,494,837,867.00
2.	H/W Moshi	Sh. 1,426,517,265.00
3.	H/M Moshi	Sh. 768,272,162.00

4.	H/W Kibaha	Sh. 643,408,950.00
5.	H/W Misungwi	Sh. 637,285,584.00
6.	H/Mji Songea	Sh. 516,356,890.00

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madeni ambayo yanapaswa kulipwa na Halmashauri, jumla ya **Sh. 56,504,070,094.62** zilibainika kutolipwa kwa muda mrefu. Orodha ya baadhi za Halmashauri zinazodaiwa kiasi kikubwa cha fedha ni kama inavyoonekana katika jedwali namba 8.

Jedwali Na. 8: Madeni ya Wazabuni yanayopaswa kulipwa na Halmashauri zaidi ya Bilioni Moja

S/N	Jina la Hamashauri	Kiasi
1.	H/Jiji Dodoma	Sh. 15,438,527,245.43
2.	H/M Ubungo	Sh. 4,721,159,136.00
3.	H/M Shinyanga	Sh. 2,680,621,701.00
4.	H/M Iringa	Sh. 2,651,017,726.00
5.	H/Jiji Mbeya	Sh. 2,041,320,251.00
6.	H/M Moshi	Sh. 2,005,880,703.00
7.	H/M Ilemela	Sh. 1,873,336,295.00
8.	H/Mji Babati	Sh. 1,492,455,569.84
9.	H/W Rungwe	Sh. 1,255,560,036.74
10.	H/W Iringa	Sh. 1,240,850,995.00

Mheshimiwa Spika, madhara ya wazabuni kutolipwa kwa wakati ni pamoja na wazabuni kufilisika, wazabuni kusitisha au kupunguza

utoaji wa huduma (kama chakula cha shule au dawa na vifaa tiba), kuongezeka kwa mzigo wa gharama za fidia na faini kupitia amri za kisheria na Sekta binafsi kusita kufanya biashara au kutoa huduma kwa Halmashauri kwa sababu ya hofu ya kucheleweshewa malipo.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano ya kina na Maafisa Masuuli, Kamati ilielezwa kuwa, Wizara ya Fedha pamoja na Halmashauri zinafanya uhakiki wa kina ili kubaini uhalali wa madeni kabla ya kuyalipa ili kuepuka madeni hewa. Aidha, Halmashauri zinaendelea kutenga fedha kwenye bajeti za kila mwaka ili kulipa malimbikizo ya madeni hayo. Kamati inazitaka Halmashauri na Wizara ya Fedha (Hazina) kuongeza nidhamu ya fedha katika ulipaji wa madeni ya wazabuni kwa kuwa, Halmashauri zimeshapata huduma kutoka kwa wazabuni hao ambao umri wa madeni wa baadhi ya wazabuni unazidi miaka Kumi.

2.3.5 Mapungufu katika utekelezaji wa miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha ustawi wa wananchi, Halmashauri zinatekeleza miradi mbalimbali katika Sekta ya Afya, Elimu, Maji, Miundombinu na Utawala. Miradi hiyo hutekelezwa kwa fedha za Serikali Kuu au Fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri. Kwa Mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2025 Serikali ilitoa jumla ya **Sh. 1,003,696,991,488.89** katika Halmashauri 75 zilizofika mbele ya Kamati kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Ili miradi hiyo iweze kuleta tija na kuongeza uwajibikaji kwa wananchi, utekelezaji wa miradi umekuwa ukisimamiwa na Sheria mbalimbali kutokana na aina ya mradi, chanzo cha fedha, na mfumo wa uendeshaji. Sheria zinazosimamia ni pamoja na Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015, Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290. Kinyume na matakwa ya Sheria hizo, mapungufu yafuatayo yamebainika katika utekelezaji wa miradi.

2.3.5.1 Kutokukamilika kwa miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ambayo Kamati imebaini ni kutokamilika kwa miradi ya maendeleo hali inayozorotesha kasi ya maendeleo. Halmashauri zimekuwa na miradi mingi ambayo haijakamilika ndani ya kipindi cha utekelezaji kilichopangwa. Aidha, ipo baadhi ya miradi ambayo imetelekezwa bila kumaliziwa hadi kufikia kipindi cha miaka Kumi. Miradi ya aina hii mingi ni ile iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi.

Baada ya majadiliano ya kina na Wakurugenzi, sababu zilizobainika za miradi kutokamilika kwa wakati ni kutotumia fedha za miradi kwa wakati, ucheleweshwaji wa fedha za miradi hali inayopelekea wakandarasi kusimamisha kazi, uwezo mdogo wa wakandarasi, usimamizi na ufuatiliaji usioridhisha wa miradi, migogoro ya ardhi pamoja na kuchelewa kwa malipo ya fidia na mabadiliko ya michoro.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zilizobainika kuwa na miradi isiyokamilika katika muda uliopangwa licha ya fedha za utekelezaji wa miradi hiyo kupokelewa ni kama inavyoonekana katika jedwali namba 9.

Jedwali Na. 9: Orodha ya Halmashauri ambao hazijakamilisha miradi kwa wakati

S/N	Jina la Hamashauri	Idadi ya Miradi Isiyokamilika	Gharama/Thamani ya mradi
1.	H/W Same	Miradi 8	Sh. 1,768,696,675.00
2.	H/M Moshi	Hospitali ya Manispaa	Sh. 5,953,358,792.00
3.	H/W Moshi	Miradi 6	Sh. 1,445,868,420.00
4.	H/W Namtumbo	Miradi 9	Sh. 1,565,972,600.00
5.	H/W Geita	Miradi 10	Sh. 1,276,000,000.00
6.	H/M Kigamboni	Miradi 44	Sh. 2,733,175,508.00
7.	H/W Bagamoyo	Miradi 17	Sh. 8,782,467,850.00
8.	H/W Busega	Miradi 63	Sh. 3,046,472,472.21
9.	H/W Missenyi	Miradi 7	Sh. 2,331,800,000.00
10.	H/W Meru	Miradi 30	Sh. 2,007,664,888.00

Mheshimiwa Spika, madhara yanayoweza kupatikana kutokana na kutokamilika kwa miradi kwa wakati ni ongezeko la gharama za miradi, mdororo wa sekta binafsi, wananchi kuchelewa kupata faida iliyotarajiwa, ukosefu wa ajira na kuharibika kwa miundombinu ya awali.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya Kamati katika taarifa za Halmashauri yamebaini uwepo wa miradi ya kimkakati ambayo

utekelezaji wake umekuwa ni wa kusuasua licha ya fedha za Umma kutumika. Miradi hiyo ni pamoja na:-

a) Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Idara ya Afya (H/Jiji Mwanza)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Jiji la Mwanza iliingia Mkataba Na. MCC/089/2011/2012/W/08 na Mkandarasi **M/s Tanzania Building Works Ltd** na Mshauri Elekezi M/s K& M Archplan (T) P.O. Box 32625 DSM kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa Ofisi za Idara ya Afya za Halmashauri (Ofisi na Stoo za Madawa) wenye thamani ya Mkataba ya **Sh. 2,108,197,292**.

Utekelezaji wa mradi huu ulianza Tarehe 20 Machi, 2012 na ulipaswa kukamilika Tarehe 20 Novemba, 2012. Tarehe ya mwisho ya nyongeza ya muda wa mkataba ilikuwa ni Tarehe 13 Agosti, 2013. Hata hivyo, hadi kuwasilishwa kwa Taarifa hii Bungeni, mradi huo umefikia **Asilimia 50** tu ya utekelezaji, mkandarasi hayupo eneo la mradi na **Sh. 982,518,403** zimekwishalipwa kwa Mkandarasi huyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mradi kusimama kwa muda wa **miaka 14**, kiasi cha **Sh. 1,125,678,889** ambacho ni fedha ya bakaa hakikuwepo katika Akaunti ya Amana wakati wa ukaguzi wa CAG mwezi Machi, 2016. Mpaka ripoti hii inakamilika, hakuna vielelezo vya matumizi ya fedha hizo wala nyaraka zozote za utekelezaji wa mradi ikiwemo Mkataba.

Kutelekezwa kwa mradi kumesababisha kupungua kwa ubora wa nondo zilizotumika kujenga nguzo za zege (Bim), Kuta za jengo

kuendelea kuharibika, kuonesha ukuaji wa fangasi na baadhi ya kuta kutengeneza nyufa na kutokurejeshwa kwa malipo ya awali (advance payment) **Sh. 527,049,323**.

Mheshimiwa Spika, wakati wa majadiliano, Afisa Masuuli aliijulisha Kamati kuwa, Halmashauri imeanza mchakato wa kumpata mtaalamu kwa ajili ya kufanya tathimini ya mradi ili kubaini uimara wake kabla ya kuendelea na ujenzi wa jengo hilo. Ripoti ya tathimini itakapokamilika, Halmashauri itaanza tena ujenzi wa jengo hilo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imemtaka Afisa Masuuli kutenga bajeti kwa ajili ya uendelezaji wa jengo hilo ili tija ya uwekezaji wa Halmashauri iweze kupatikana.

b) Mradi wa Stendi ya Mabasi Ngangamfumuni (H/M Moshi)

Mheshimiwa Spika, tarehe 28/1/2019, H/M Moshi iliingia Mkataba Na. LGA/045/2018–2019/HQ/W/13 na M/s CRJE (East Africa) Limited kwa ajili ya ujenzi wa Stendi ya Mabasi ya Ngangamfumuni kwa gharama ya **Sh. 19,932,910,740**. Mwezi Disemba, 2025, Halmashauri ilipokea jumla ya **Sh. 10,182,231,438.15** ambapo, **Sh. 9,522,449,438.15** ni kutoka Hazina na **Sh. 659,782,000** ni kutoka katika mapato ya ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Licha ya kuwa Tarehe ya mwisho ya ukamilishaji wa mradi iliyorejewa ni 26 Aprili 2026, utekelezaji wa mradi huo ulisimama Tarehe 15/5/2022 hadi Tarehe 20 Juni, 2026 kutokana na ukosefu wa fedha na kazi zenye thamani ya **Sh.**

7,240,274,013 zilitekelezwa sawa na **Asilimia 36.3** ya gharama zote za mradi na kubakiwa na kazi za **Sh. 12,692,636,727**.

Mheshimiwa Spika, Baada ya kufanyika kwa marekebisho ya wigo wa kazi, kazi zenye thamani ya **Sh. 5,254,519,748** ziliondolewa, ambapo kazi zilizobaki za **Sh. 7,438,116,979** zilipangwa kutekelezwa kwa gharama ya **Sh. 12,366,022,946** na kusababisha gharama za mradi kuongezeka kwa **Sh. 5,606,652,391**.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mradi kusimama kutokana na ukosefu wa fedha, Mkataba ulikuwa na Kifungu kilichosema kuwa, endapo mkataba hautakamilika ndani ya miezi 30, yatafanyika mabadiliko ya bei kwa kutumia viwango vipya. Aidha, Kifungu hicho hakikuwepo kwenye nyaraka ya tenda bali kiliwekwa kwenye muhtasari wa majadiliano (negotiation minutes).

Kuendelea kuchelewa kwa utekelezaji wa mradi huu, kunazidi kuongeza hatari ya kuongezeka kwa gharama za mradi kwa kuwa, hadi kuwasilishwa kwa taarifa hii ya Kamati, mradi huu bado haujakamilika. Kamati inaitaka Wizara ya Fedha kutoa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa mradi huu.

c) Mradi Ujenzi wa Wodi ya Upasuaji (H/Mji Tunduma)

Mheshimiwa Spika, kila Halmashauri inapaswa kufanya upembuzi yakinifu kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi wowote ili miradi iweze kukamilika kwa wakati. Kinyume na Kanuni ya 309 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024, Halmashauri iliingia Mkataba Na. 78J10/2023/2024/W/119 na Mkandarasi M/S Hamerkop International

Ltd kwa ajili ya ujenzi wa wodi na chumba cha upasuaji (Block B) katika Hospitali ya Mji.

Kwa mujibu wa Mkataba, mradi huu ulianza kutekelezwa Tarehe 4 Oktoba, 2024 kwa gharama ya **Sh. 2,344,886,350** bila kujumuisha kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Utekelezaji wa mradi huu uliotarajiwa kukamilika Tarehe 3 Julai, 2025 umekuwa ni wa kusuasua. Aidha, ukaguzi uliofanywa na CAG Tarehe 29 Julai, 2025 ulibaini mradi kutokamilika kwa wakati na ujenzi ulifikia hatua ya msingi ambapo sehemu moja imemiminwa bamba la zege (Concrete Slab).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, kutokamilika kwa mradi huu kunatokana na uwezo mdogo wa Mkandarasi. Kamati inaitaka Halmashauri kuongeza ufuatiliaji wa miradi na kufanya upekuzi kabla ya kutoa kazi kwa wakandarasi ili mradi huu uweze kukamilika kwa haraka kwa kuwa muda wa utekelezaji ulishakamilika na Mkandarasi alishalipwa **Sh. 351,732,952** ambayo ni malipo ya awali.

d) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Mafuta Kata ya Somangila (H/M Kigamboni)

Mheshimiwa Spika, Tarehe 20 Juni, 2024, Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ilianzisha mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mafuta katika Kata ya Somangila kwa gharama ya **Sh. 1,361,578,600** na mradi ulitarajiwa kukamilika Tarehe 19 Juni, 2025. Mradi huu ulitekelezwa na Mkandarasi Prince General Investment Ltd kwa Mkataba Na. 88Z5/2023/2024/W/22.

Utekelezwaji wa mradi huu ulikumbwa na changamoto mbalimbali zilizosababisha kuchelewa kwa muda wa **siku 186**. Changamoto zilizobainika ni kutowasilishwa kwa taarifa za maendeleo ya mradi na mkandarasi, uwepo wa vipengele vinavyojirudia kwenye BOQ bila maelezo ya msingi, pamoja na kutowasilishwa kwa nyaraka za matumizi ya malipo ya awali (Advance Payment)

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi alianza kazi bila ya kuwa na Cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira (Environmental Impact Assessment Certificate), kibali cha ujenzi, kibali kutoka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, kibali cha Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) pamoja na kibali cha kuunganisha Barabara kinyume na Sheria.

Mheshimiwa Spika, hadi Kamati ilipokutana na Halmashauri, Mkandarasi alikwishalipwa jumla ya **Sh. 437,776,241** na mkataba umesitishwa. Kusitishwa kwa utekelezaji wa mradi kunachelewesha upatikanaji wa huduma kwa jamii pamoja na upotevu wa fedha za umma ambazo zimeshatolewa kwa Mkandarasi. Kamati imemtaka Afisa Masuuli kurekebisha dosari zote za kimkataba ili mradi uweze kukamilika.

e) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Biashara Manzese (H/M Ubungo)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri iliingia Mkataba na Mkandarasi Luvisa Investment Co. Limited kwa ajili ya ujenzi wa jengo la biashara Manzese kwa Mkataba Na. LGA/180/2022-2023/W/14

wenye gharama ya **Sh. 1,368,989,980**. Utekelezaji wa mradi huu ulianza tarehe 26 Juni, 2023 na kutarajiwa kukamilika Tarehe 28 Februari, 2024.

Mheshimiwa Spika, licha ya muda wa utekelezaji kuongezwa mara Nne, mradi huu bado haujakamilika na jumla ya **Sh. 1,076,544,331** zimeshalipwa kwa Mkandarasi na Mkandarasi ametelekeza mradi kwa zaidi ya miezi mitano. Sababu za mradi kutokamilika kwa wakati ni mapungufu katika usimamizi na ufuatiliaji na Mkandarasi kushindwa kutekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, Wakati wa mahojiano, Kamati ilielezwa kuwa, Halmashauri imemuandikia barua Mkandarasi na ina mpango wa kusitisha Mkataba ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa. Kamati imemtaka Afisa Masuuli kuchukua hatua za haraka ili mradi huu uweze kukamilika ili fedha za umma zinawanufaishe wananchi.

f) Mradi wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri (H/W Sikonge)

Mheshimiwa Spika, Mwaka wa fedha 2009/2010, Halmashauri ilianza ujenzi wa makao makuu ya Halmashauri kwa makadirio ya **Sh. Bilioni 5.6**. Fedha za utekelezaji wa mradi zilikuwa zikitolewa kwa awamu na Hazina na baadae upatikanaji wa fedha ukasimama. Hata hivyo, hapakuwa na Tarehe maalumu ya ukamilishaji wa mradi huu kwa kuwa, Halmashauri ilikuwa ikiingia mikataba na mafundi pindi tu fedha inapopatikana.

Mheshimiwa Spika, Licha ya **Sh. 4,872,447,818** kati ya **Sh. 5,230,117,551** zilizopokelewa kuwa zimekwishatumika, mradi huu haujakamilika na umeshachukua takriban **miaka 16**. Kamati ilielezwa kuwa, mradi huu umeshindwa kukamilika kwa wakati kutokana na kukosekana kwa fedha za ukamilishaji. Aidha, Afisa Masuuli amemuandikia Katibu Tawala Mkoa (RAS) kuwa kiasi cha **Sh. 1,485,094,980** kinahitajika ili kukamilisha mradi huu.

Pamoja na maelezo yaliyotolewa, Kamati haijaona mikakati ya umaliziaji wa mradi huu ili jengo hilo liweze kukamilika na thamani ya fedha iweze kupatikana. Halmashauri inashauriwa kuwa na mipango madhubuti ya umaliziaji wa mradi huu.

g) Taasisi za Serikali (SUMA JKT) kuchelewesha utekelezaji wa Miradi

Mheshimiwa Spika, Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT) limekuwa likipewa dhamana ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo inayojumuisha ujenzi wa majengo ya utawala, vituo vya afya na shule. Halmashauri zimekuwa zikilitumia Shirika hili kutokana na misingi ya uaminifu, uadilifu na uzalendo pamoja na uwezo wa kiufundi.

Mheshimiwa Spika, Katika kupitia utekelezaji wa miradi, Kamati imebaini SUMA JKT kutokamilisha miradi yake katika kipindi kilichoainishwa katika mkataba. Changamoto hizo zilibainika wakati wa kupitia taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za H/W Same, H/W Bunda na H/W Msalala.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Same, Tarehe 23 Aprili 2024, Halmashauri iliingia Mkataba wa **Sh. 376,633,788** na SUMA JKT Construction Ltd kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi Mtendaji na kutarajiwa kukamilika Tarehe 24 Oktoba, 2024. Pamoja na Tarehe ya ukamilishaji wa mradi ilisogezwa hadi Tarehe 26 Septemba, 2025 mradi huu bado haujakamilika. Hadi ukaguzi wa eneo la mradi tarehe 3 Septemba, 2025, utekelezaji ulikuwa umefikia **Asilimia 10** pekee, huku siku 497 sawa na Asilimia 95.6 ya muda wa mkataba zikiwa zimepita.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda iliingia mkataba wa ujenzi wa jengo la makao makuu ya Halmashauri na Kampuni ya SUMA JKT tarehe 7 Juni, 2021 kwa gharama ya nguvukazi ya **Sh. 587,130,994** na kukadiriwa kugharimu **Sh. 3,578,773,698.41**. Ujenzi huo haukukamilika licha ya kupokelewa na kutumika kwa **Sh. 3,000,000,000** kutoka Hazina na kumalizika kwa muda mkataba tarehe 3 Juni 2024.

Kamati imebaini mapungufu kadhaa katika utekelezaji wa mradi huu ambayo ni pamoja na Mkandarasi kutelekeza mradi bila ya kuhuisha mkataba na uchepushaji wa vifaa vya ujenzi wa mradi, ikiwemo mifuko 400 ya saruji yenye thamani ya **Sh. 8,200,000**, ambapo mifuko 300 yenye thamani ya **Sh. 6,500,000** haikurejeshwa baada ya ajali.

Mheshimiwa Spika, Mifuko mingine 600 ya saruji yenye thamani ya **Sh. 12,300,000** ilikopeshwa kwa SUMA JKT; matofali 5,400 ya saruji yenye thamani ya **Sh. 7,560,000** yalikopeshwa kwa VETA,

ambapo matofali 712 yenye thamani ya **Sh. 996,800** bado hayajarejeshwa; mifuko 110 ya saruji yenye thamani ya **Sh. 2,530,000** iliganda; pamoja na kutotayarishwa kwa taarifa za maendeleo ya mradi za lazima za kila wiki na kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, changamoto kama zilizotokea katika katika Halmashauri tajwa hapo juu ilitokea pia katika H/W Msalala ambapo, Halmashauri iliingia mkataba na SUMA JKT (Na. LGA/163/2016-17/CDG/W/61) kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri wenye thamani ya **Sh. 4,314,837,383**. Mradi ulitarajiwa kukamilika ndani ya miezi 12 kuanzia tarehe 7 Juni, 2017. Hata hivyo, hadi Agosti 2025 mradi haukuwa umekamilika, mkataba ulikuwa umeisha muda na mkandarasi hakuwepo eneo la mradi.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kuchelewa kukamilika kwa mradi huo, Halmashauri haikutoza *liquidated damages* kutokana na kuchelewa kukamilisha mradi. Aidha, Halmashauri ilishindwa kurejesha kiasi cha **Sh. 355,815,010** kilichotolewa kwa Mkandarasi kama malipo ya awali licha ya mkataba kuisha muda.

Mheshimiwa Spika, Kamati haijaridhishwa na utekelezaji wa miradi hiyo na kuitaka SUMA JKT kukamilisha matakwa ya kimkataba ili kuongeza imani ya Halmashauri kwa Taasisi hiyo ya Serikali na miradi hiyo iweze kukamilika muda uliopangwa kwa ajili ya maslahi mapana ya Taifa.

2.3.5.2 Halmashauri kutotenga mapato ya Ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kipengele cha 4.4.1 cha Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/2025 umetoa maelekezo mahususi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa juu ya kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kulingana na uwezo wa Halmashauri hizo. Sheria, Kanuni na Miongozo imewekwa ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma sahihi katika muda sahihi. Katika mwaka wa fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2025, Halmashauri zote hazikutenga mapato ya ndani yenye jumla ya **Sh. 22,697,054,616** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Uchambuzi wa Kamati umebaini sababu mbalimbali zinazosababisha Halmashauri nyingi kutotenga fedha kutoka katika mapato ya ndani ambazo ni mapato ya ndani kutumika katika matumizi mengineyo (recurrent expenditure) ambayo tayari yana bajeti zake, upungufu wa mapato ya ndani kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kutozingatiwa kwa matakwa ya Sheria, Kanuni na Miongozo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri kutotenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kunasababisha miradi ya kimkakati kutokamilika kwa wakati hali inayopelekea huduma kushindwa kuifikia jamii na kwa wakati uliopangwa. Athari nyingine ni kuongezeka kwa gharama za miradi kunakotokana na bei za vifaa kubadilika na wananchi kukosa imani na Serikali haswa kwa miradi iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi inaposhindwa kukamilishwa na Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, katika kujiridhisha iwapo kuna mazingatio ya Sheria na fedha za umma zinatumika kwa usahihi, Kamati imekuwa ikichambua fedha za miradi ya maendeleo ambazo hazikupelekwa ndani ya miaka mitatu 2022/2023 hadi 2024/2025 ili kufahamu ukubwa wa tatizo lililopo. Kwa Halmashauri 75, jumla ya **Sh. 43,498,700,308.69** kutoka mapato ya ndani hazikupelekwa katika miradi ya maendeleo. Orodha ya baadhi ya Halmashauri ambazo hazikupeleka fedha zote za miradi ya maendeleo kwa mujibu wa Sheria imeoneshwa katika jedwali namba 10.

Jedwali Na. 10: Halmashauri ambazo hazikupeleka fedha zote za miradi ya maendeleo kutoka katika mapato ya ndani

Jina la Hamashauri	Kiasi kilichopaswa kupelekwa (3 yrs)	Kiasi kilichopelekwa (3 yrs)	Kiasi ambacho hakikupelekwa (3yrs)
H/Jiji Tanga	27,510,918,988.00	20,644,925,839.00	6,865,993,149.00
H/Jiji Mwanza	35,076,153,143.00	29,299,787,724.00	5,776,365,419.00
H/Jiji Dodoma	55,123,359,613.00	49,446,060,776.00	5,677,298,837.00
H/W Mbozi	9,453,425,677.00	5,068,854,397.00	4,384,571,278.00
H/M Singida	6,522,105,905.00	4,330,097,378.00	2,192,008,527.00
H/M Shinyanga	8,029,077,928.00	6,006,513,357.00	2,022,564,571.00

Mheshimiwa Spika, Maafisa Masuuli wameieleza Kamati kuwa, ufinyu wa fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo ndio uliosababisha kutumika kwa fedha za miradi kinyume na Sheria. Kamati inazitaka Halmashauri zote kuzingatia Sheria ya upelekaji wa fedha za miradi ya maendeleo ndani ya mwaka wa fedha husika na kulipa madeni yote ya nyuma.

2.3.5.3 Utekelezaji hafifu wa majukumu wa wajibu wa makampuni kwa jamii (CSR)

Mheshimiwa Spika, Kanuni za wajibu wa wamiliki wa leseni za madini kwa jamii za Mwaka 2023 zinaelezea na kusimamia wajibu wa kampuni na wawekezaji wa sekta ya madini katika kuchangia maendeleo ya jamii zinazozunguka maeneo ya migodi (Corporate Social Responsibility – CSR). Kinyume na matakwa ya Kanuni hizo, uchambuzi wa Kamati wa ripoti ya CAG umebaini kuwa, wamiliki wa leseni za madini hawatekelezi wajibu wao kikamilifu kwa jamii. Vile vile, Halmashauri hazitekelezi wajibu wao kikamilifu kinyume na majukumu yaliyoainishwa katika Kanuni hizo.

Sababu za Kanuni hizo kutofuatwa ni udhaifu wa Halmashauri katika usimamizi na ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya kijamii pamoja na ushirikishwaji duni wa viongozi wa Halmashauri katika uandaaji wa mpango. Halmashauri zilizobainika kuwa na changamoto hiyo zimeoneshwa katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 11: Kampuni zisizotekeleza wajibu kwa jamii (CSR)

Jina la Hamashauri	Jina la Kampuni yenye leseni ya Madini	Mwaka	Miradi ambayo utekelezaji haujaanza	Miradi ambayo utekelezaji haujakamilika
H/M Geita	GGML	2022, 2023 na 2024	Miradi 4 yenye thamani ya Sh. 3,530,553,684	Miradi 11 yenye thamani ya Sh. 1,517,684,881.96
H/W Kishapu	Williamson Diamond Ltd	2023/24 na 2024/25	Miradi 11 yenye thamani ya Sh.1,230,000,000	Sh. 680,000,000

Jina la Hamashauri	Jina la Kampuni yenye leseni ya Madini	Mwaka	Miradi ambayo utekelezaji haujaanza	Miradi ambayo utekelezaji haujakamilika
H/Jiji Tanga	Tanga Cement Company, Neelkanth Company Limited, New Port Minerals na Kilimanjaro Cement	Kampuni hizi hazikushiriki katika mashauriano na Halmashauri, hazikuwasilisha mipango ya CSR kwa ajili ya idhini, wala kushiriki katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi		

Mheshimiwa Spika, Kampuni zinazomiliki leseni za madini kushindwa kutimiza wajibu wake kwa jamii zinasababisha kutotekelezwa kwa miradi ya maendeleo kwa jamii, upotevu wa mapato ya Halmashauri kupitia uwekezaji wa Makampuni hayo. Vile vile, kunakosesha wananchi fursa za ajira na kupungua kwa mzunguko wa fedha kwa jamii hasa watoa huduma wa ndani (Local Content), kuongezeka kwa migogoro kati ya wananchi na wachimbaji na uharibifu wa mazingira bila faida.

Mheshimiwa Spika, iwapo Mamlaka husika hazitachukua hatua stahiki za uboreshaji wa utekelezaji wa wajibu kwa jamii, faida na tija ya uwekezaji katika maeneo yao hayataonekana. Kamati inazielekeza Mamlaka husika kusimamia matakwa ya Kanuni na kuhakikisha kilichokusudiwa kinawafikia wananchi.

2.3.6 Mapungufu katika Usimamizi wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikifanya uchambuzi wa fedha za Mfuko wa Wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kujiridhisha iwapo kanuni zinazohusu upangaji, utekelezaji, usimamizi na ufuatiliaji wa mfuko huo zinafuatwa kikamilifu kwa maslahi mapana ya walengwa wa Mfuko huo.

Maeneo mahususi yaliyoangaliwa na Kamati ni wajibu wa Halmashauri katika kutenga fedha za mapato ya ndani katika mfuko huo, utaratibu na ufanisi katika ugawaji wa fedha za vikundi, uwazi na uwajibikaji wa usimamizi wa mfuko, uhalali wa vikundi husika pamoja na urejeshwaji wa fedha zilizokopeshwa kwa vikundi. Ufafanuzi wa kina wa maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

2.3.6.1 Fedha za Mapato ya Ndani kutowasilishwa katika Mfuko wa Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu Sh. 13,882,521,799

Mheshimiwa Spika, uchangiaji wa Asilimia 10 kutoka katika mapato ya ndani kwenda kwenye Mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu umeelezwa katika Kifungu cha 37(A) cha Sheria ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sura ya 290. Hata hivyo, wajibu wa Halmashauri katika kukidhi matakwa ya Sheria hiyo umekuwa si wenye kutekelezwa kikamilifu ambapo, katika Mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2025, Jumla ya **Sh. 13,882,521,799** hazikupelekwa katika Mfuko wa wanawake, vijana

na watu wenye ulemavu licha ya fedha hizo kukusanywa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, baada ya mahojiano na Halmashauri, Kamati imebaini Halmashauri nyingi kutopeleka kikamilifu Asilimia 10 ya mapato ya ndani katika Mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Katika Halmashauri 75 zilizofika mbele ya Kamati, Jumla ya **Sh. 10,004,802,885.88** hazikuwasilishwa katika mfuko kwa muda wa miaka mitatu.

Kushindwa kupelekwa kwa fedha hizo kunatokana na Halmashauri kutoweka kipaumbele katika upelekaji wa fedha katika mfuko huo. Halmashauri ambazo hazikupeleka kikamilifu fedha za Mfuko kwa kiasi kikubwa kwa miaka mitatu mfululizo ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 12: Halmashauri ambazo hazikuchangia kikamilifu katika Mfumo wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa miaka mitatu (2022/2023 hadi 2024/2025)

Jina la Halmshauri	Kiasi kilichopaswa kuchangiwa (3yrs)	Kiasi halisi kilichochangiwa (3yrs)	Pungufu (3yrs)
H/Jiji Mwanza	5,488,521,455.00	3,766,000,000.00	1,722,521,455.00
H/M Shinyanga	1,018,745,334.00	359,573,877.00	659,171,457.00
H/Jiji Tanga	4,114,858,703.00	3,673,266,454.00	441,592,249.00
H/W Mbozi	1,711,811,100.00	1,335,364,533.00	376,446,567.00
H/M Musoma	555,080,821.00	249,845,086.00	305,235,735.00

Mheshimiwa Spika, Maafisa Masuuli waliijulisha Kamati kuwa, fedha ambazo hazikupelekwa katika Mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu zilitumika katika matumizi mengineyo. Athari za kutowasilishwa kwa wakati kwa fedha za Mfuko huo ni walengwa kukosa fursa ya kupata mitaji ya kuanzisha au kuendeleza biashara ndogo na za kati, kudorola kwa uchumi na kuongezeka kwa wimbi la umasikini katika jamii na matumizi mabaya ya fedha ambazo zilipaswa kutumika katika vikundi. Kamati imekuwa ikizielekeza Halmashauri zote kuwasilisha fedha hizo katika mfuko.

2.3.6.2 Mikopo iliyotolewa katika Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kutorejeshwa Sh. Bilioni 120.48

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kusimamia na kufuatilia utoaji wa mikopo kwa kuzingatia Kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu za mwaka 2024. Pamoja na mambo mengine, mambo muhimu yaliyozingatiwa na Kamati katika eneo hili ni mgao wa fedha za mikopo, sifa za waombaji, muda wa mkopo kuanza kurejeshwa, makosa na adhabu zake.

Katika kuhakikisha fedha zilizokopeshwa kwa vikundi zinarejeshwa ndani ya muda uliopangwa ili ziweze kuwanufaisha walengwa wengine, Kamati ilihoji kuhusu sababu za msingi zinazosababisha sehemu kubwa ya mikopo iliyotolewa kwa vikundi kutorejeshwa kwa wakati.

Sababu zilizobainika za mikopo kutorejeshwa kwa wakati ni kutofanyika kwa tathimini ya kina ya aina ya vikundi vinavyopewa mikopo, aina ya biashara inayotaka kufanyika kwa fedha za mkopo na utayari wa wana kikundi kurejesha mkopo huo. Vile vile, sababu nyingine ni kutotolewa kwa elimu ya kutosha kwa wananchi kuhusu mikopo hiyo, uwepo wa vikundi hewa vilivyopewa mikopo na Maafisa Maendeleo ya Jamii kutofanya ufuatiliaji wa vikundi vilivyopewa mikopo kulikosababisha vikundi hivyo kusambaratika bila Halmashauri kuwa na taarifa mapema.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, jumla ya Sh. **Bilioni 120.48** zilizotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu hazikukusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hata hivyo, kwa Halmashauri 75 zilizofika mbele ya Kamati na pamoja na juhudi za ukusanyaji wa fedha hizo kuendelea, jumla ya **Sh. 59,600,904,613.46** zilikuwa hazijarejeshwa na vikundi. Baadhi ya Halmashauri ambazo hazikukusanya kiasi kikubwa cha fedha ni kama inavyoonekana katika jedwali.

Jedwali Na. 13: Halmashauri ambazo hazijakusanya mikopo iliyotolewa katika vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu zaidi ya Bilioni 1

S/N	Jina la Halmashauri	Kiasi
1.	H/Jiji Dodoma	Sh. 5,881,905,742.00
2.	H/M Ubungo	Sh. 5,831,918,876.44
3.	H/Jiji Mwanza	Sh. 3,626,024,170.00
4.	H/Jiji Tanga	Sh. 2,314,462,433.00

S/N	Jina la Halmashauri	Kiasi
5.	H/Mji Tunduma	Sh. 2,220,695,070.00
6.	H/M Kigamboni	Sh. 1,810,269,634.00
7.	H/W Kibaha	Sh. 1,377,823,665.00
8.	H/M Songea	Sh. 1,353,045,214.00
9.	H/M Geita	Sh. 1,344,734,706.00
10.	H/W Tarime	Sh. 1,343,081,625.00

Mheshimiwa Spika, mahojiano na Maafisa Masuuli yameisaidia Kamati kubaini kutokuwepo kwa ufuatiliaji wa karibu wa vikundi kwa kuwa, baadhi ya Maafisa Maendeleo ya Jamii hawana taarifa juu mahali walipo wajumbe wa baadhi ya vikundi vilivyopewa mkopo na hakuna biashara inayoendelea.

Mheshimiwa Spika, Athari ya vikundi vilivyokopeshwa fedha kutorejesha kwa wakati ni vikundi vipya kukosa fursa ya kukopa, upotevu wa fedha za umma na Halmashauri kushindwa kutimiza malengo yake ya kisheria ya kuwainua wananchi kiuchumi kupitia Asilimia 10 ya mapato yake ya ndani. Kamati inazitaka Halmashauri kuchukua hatua stahiki za kisheria kwa vikundi vyote vitakavyoshindwa kurejesha fedha hizo kwa wakati.

2.3.6.3 Kutozingatiwa kwa Uwiano wa Ugawaji wa Mikopo Katika Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu (4:4:2)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo ya vikundi vya

wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, Mamlaka ya Serikali za Mtaa zinapaswa kutoa mikopo kwa kuzingatia uwiano wa 4:4:2 ili makundi yote yaweze kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa ya CAG na kufanya mahojiano na Maafisa Masuuli (Wakurugenzi) wa Halmashauri waliofika mbele ya Kamati na kubaini kuwa Halmashauri nyingi hazizingatii uwiano wa 4:4:2 kama Kanuni ilivyoelekeza. Changamoto hiyo inatokana na Maafisa Maendeleo ya Jamii kutofanya kazi yao ya kutoa elimu ipasavyo hasa katika kuwafikia na kuwatambua watu wenye ulemavu. Mfano wa Halmashauri ambazo hazikuzingatia uwiano wa 4:4:2 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni kama inavyoonekana katika jedwali.

Jedwali Na. 14: Halmashauri ambazo hazikuzingatia uwiano wa 4:4:2

S/N	Jina la Halmashauri	Kiasi kilichotolewa	Wanawake: Asilimia 40	Vijana: Asilimia 40	Watu wenye ulemavu: Asilimia 20
1	Bukoba MC	749,364,898	57	42	2
2	Mpanda DC	939,824,000	50	46	4
3	Meru DC	1,307,037,985.5	49	47	4
4	Arusha DC	1,363,452,500	53	42	5
5	Namtumbo Dc	591,336,732	52	42	6

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 53 cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 iliyofanyiwa marekebisho imeruhusu Halmashauri kutumia fedha iliyosalia ya Kundi ambalo maombi ya fedha hayakupokelewa kwa ajili ya Kundi lingine lenye mahitaji zaidi. Hata hivyo, mabadiliko hayo yanapaswa kuidhinishwa na timu ya Menejimenti ya Halmashauri baada ya

kujiridhisha kuwa, juhudi za uhamasishaji zimefanyika na Kundi husika halikujitokeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini ukiukwaji wa Sheria na Kanuni ambapo, Halmashauri nyingi zimekuwa zikitoa kipaumbele kwa vikundi vya wanawake ikilinganishwa na vikundi vya vijana na watu wenye ulemavu bila ya kuzingatia kifungu tajwa hapo juu. Maafisa Masuuli wamekuwa wakiieleza Kamati kuwa, sababu ya vikundi vya wanawake kupewa mikopo kwa asilimia kubwa kunatokana na vijana na watu wenye ulemavu kutojitokeza kwa ajili ya uchukuaji wa mikopo.

Kamati imeona changamoto hiyo inatokana na mapungufu ya kiutendaji ya Maafisa Maendeleo ya Jamii katika kuhakikisha watu wote waliokusudiwa wanapata fursa inayofanana. Vile vile, Kamati imezitaka Halmashauri zote kuhakikisha utoaji wa mikopo unazingatia uwiano wa kisheria kwa kuwa, kuna Kundi kubwa la vijana ambalo halipewi fursa ya mikopo hiyo.

2.3.6.4 Gharama za ukusanyaji wa mikopo kuwa kubwa zaidi ya kiwango kinachokubalika

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 38 (1) ya Kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo ya Asilimia 10, Halmashauri inatakiwa kutenga kiasi kisichozidi Asilimia 15 kama sehemu ya mafunzo pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya mikopo iliyokopeshwa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Katika uchambuzi wa ripoti ya CAG uliofanywa na Kamati umebaini kuwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimejitahidi kuwekeza katika

vitendeakazi ikiwa ni pamoja na ununuzi wa magari na pikipiki kwa ajili ya ufuatiliaji. Kamati inaunga mkono juhudi hizi za kuongeza vitendea kazi ili kuwezesha kufikiwa kwa walengwa wengi zaidi na kwa wakati. Hata hivyo Kamati inaona kuwa matumizi ya rasilimali hizi yazingatie thamani ya fedha.

Mheshimiwa Spika, Kamati inazikumbusha Halmashauri kuzingatia Sheria na Kanuni ili gharama zinazotumika kukusanya mikopo zisizidi kiwango kilichowekwa kisheria ili makusanyo halisi ya mfuko yaweze kuleta tija iliyokusudiwa kwa makundi yote katika jamii. Mfano wa Halmashauri zilizozidisha kiwango cha gharama za ufuatiliji inaonekana katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 15: Halmashauri zilizozidisha fedha za ufuatiliaji 2024/2025

Halmashauri	**Mikopo iliyotolewa**	**Asilimia ya ufuatiliaji iliyotakiwa (15%)**	**Kiasi kilicho tumika**	**Asilimia ya iliyotumika**
H/W Moshi	306,704,014	46,005,602	157,945,800	243
H/W Same	258,474,831	38,771,225	53,269,966	20.6

2.3.7 Kukosekana kwa mipango sahihi ya uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mheshimiwa Spika, ili kupata vyanzo mbadala vya mapato endelevu, rasilimali za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuwekezwa katika miradi inayotekelezeka na yenye tija. Ufafanuzi zaidi umetolewa katika Agizo la 52 (1) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya 2009. Kwa muktadha huo, baadhi ya Halmashauri zimefanya uwekezaji katika ujenzi wa masoko ya kisasa, stendi za

mabasi, uwekezaji katika viwanja vya mpira na uwekezaji wa majengo ya vitegauchumi, kumbi za mikutano, hoteli, na maduka (malls).

Wakati wa kupitia taarifa za fedha za Halmashauri kwa mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2025, Kamati pia ilijielekeza katika kuangalia iwapo uwekezaji uliofanywa na Halmashauri unaleta tija iliyosudiwa. Mapungufu yaliyobainika katika utekelezaji wa miradi ya uwekezaji ni kama ifuatavyo:-

2.3.7.1 Changamoto za Uwekezaji katika Masoko

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Halmashauri zimejenga masoko ya kisasa ili kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato. Hata hivyo utendaji wa masoko hayo umekuwa si wa kuridhisha ikilinganishwa na matarajio yaliyowekwa wakati wa uanzishwaji wa miradi hiyo na kukosekana kwa thamani ya fedha (value for money) kinyume na Kanuni ya 7(1) ya Kanuni za Fedha za Umma (Usimamizi wa Mali za Umma), 2024.

Kutofanya vizuri kwa masoko hayo kunatokana na changamoto mbalimbali kama kutofanyika vizuri kwa upembuzi yakinifu ili kubaini mahitaji halisi ya wananchi kabla ya kuanza kwa ujenzi, wananchi wa maeneo husika na wafanyabiashara kutoshirikishwa ipasavyo katika hatua za awali, ujenzi kufanyika katika maeneo ambayo hayapo rafiki kibiashara na ushindani mkubwa kutoka kwa wafanyabiashara walio nje ya maeneo ya masoko hayo.

Mheshimiwa Spika, Mfano ya changamoto ya masoko imeonekana katika H/Jiji Dodoma ambapo Mwaka 2022, Halmashauri ilijenga soko la kisasa la Job Ndugai kwa gharama ya **Sh. Bilioni 14.6** lengo likiwa ni kuongeza mapato ambapo, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Halmashauri ilikadiria kukusanya jumla ya **Sh. Milioni 443.2**. Ukaguzi uliofanywa na CAG Tarehe 27 Septemba, 2025 ulibaini **Asilimia 99** ya maduka (104 kati ya 105) na **Asilimia 61** ya vizimba (222 kati ya 365) kutokuwa na wapangaji.

Kukosekana kwa wapangaji kumesababisha mapato ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kushuka hadi kufikia **Sh. Milioni 89.8** ikiwa ni pungufu ya **Sh. Milioni 353.4** sawa na **Asilimia 80** ikilinganishwa na makadirio.

Mheshimiwa Spika, soko la Ndugai kutotumika kikamilifu kunaongeza gharama za uendeshaji wa soko hilo ikiwa ni pamoja na gharama za ukarabati pamoja na kuikosesha Halmashauri mapato. Gharama hizo zimekuwa zikiongezeka licha ya mapato ya soko kupungua. Kamati inaishauri Halmashauri kufanya upya tathimini ya uwekezaji uliofanyika katika soko la Ndugai.

2.3.7.2 Mapungufu ya Uwekezaji katika Vituo vya Mabasi

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya uwekezaji katika vituo vya mabasi ili kuongeza fursa za biashara katika vituo vya mabasi, kuongeza utoaji wa huduma bora kwa jamii na kuongeza mapato ya Halmashauri husika. Uwekezaji katika maeneo hayo

hufanyika kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 6(1)(k) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290.

Katika dhana ya kusimamia matumizi ya fedha za umma, Kamati imefanya uchambuzi wa ufanisi wa uendeshaji wa vituo vya mabasi. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini changamoto za kiuendeshaji zinazosababisha vituo vya mabasi kutofanya kazi kikamilifu. Changamoto hizo ni pamoja na mabadiliko ya Kanuni na Miongozo ya uendeshaji wa vituo hivyo na usimamizi usioridhisha wa vituo hasa katika utozaji wa tozo na ushuru mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kutofanya vizuri kwa vituo vya mabasi kumebainika katika H/M Ubungo ambapo, stendi ya mabasi ya Magufuli imekumbwa na changamoto za kiundeshaji kutokana na udhaifu wa mifumo ya kiusalama na hitilafu za kimuundo katika miundombinu muhimu ya kituo hali inayoathiri ufanisi wa uendeshaji na utoaji wa huduma. Kamati imeilekeza Halmashauri kuhakikisha mapungufu yote yaliyobainishwa yanaondolewa.

Pamoja na mambo mengine, H/M Ubungo pia ina changamoto ya kiuchumi kutokana na **Mabasi 1,388** sawa na **Asilimia 87** ya mabasi yote **1,595** yaliyopewa kibali cha kutumia stendi hiyo kutotumia kituo hicho kwa ajili ya kushusha na kupakia abiria. Licha ya juhudi ambazo zimechukuliwa na Serikali katika kuhakikisha Stendi ya mabasi Magufuli inafanya kazi kwa ufanisi, **Asilimia 87** ya mapato ambayo yangekusanywa katika mwaka wa fedha 2023/2024 yalipotea.

Mheshimiwa Spika, mapungufu mengine katika uwekezaji wa stendi za mabasi yalibainika katika stendi ya mabasi ya nanenane katika H/Jiji Dodoma. Kutofanya kazi kikamilifu kwa stendi hiyo kumesababisha Halmashauri kutokukusanya mapato ya **Sh. 2,000,072,594** sawa na **Asilimia 64** ya bajeti ya makusanyo ya **Sh. 3,127,343,999**.

Mheshimiwa Spika, Kamati inazitaka Halmashauri zote kufanya upembuzi wa kina kabla ya kuanzisha vituo vipya vya mabasi ili kubaini fursa ya biashara katika maeneo hayo na tija ya uwekezaji iweze kupatikana.

2.3.7.3 Kutelekezwa kwa Mradi wa Uwanja wa Mpira

Mheshimiwa Spika, tarehe 2 Julai, 2021 H/M Geita iliingia mkataba na Kampuni ya M/s EFQ Company Ltd kwa ubia na Mugogo Construction Company Ltd kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu wa Geita awamu ya kwanza kwa gharama ya **Sh. 2,407,569,050.81.** Utekelezaji wa mkataba huu ulitarajiwa kukamilika tarehe 16 Mei 2022 na baada ya muda kuongezwa mkataba ulipaswa ukamilike tarehe 15 Agosti 2022.

Hata hivyo, hadi CAG alipofanya ukaguzi katika mradi huu mwezi Septemba, 2025, mradi huu ulikuwa haujakamilika na utekelezaji wake umechukua takriban miezi 38 na jumla ya **Sh. 2,170,794,536** zilikwishatumika. Baada ya mradi kutelekezwa kwa muda mrefu Afisa Masuuli aliieleza Kamati kuwa, GGML kupitia Mshauri Elekezi NORPLAN (T) Ltd, ilifanya upembuzi yakinifu pamoja na tathmini za

kiufundi na kifedha na kubaini kuwa, **Sh. 9,579,845,957.56** zinahitajika kukamilisha mradi huu zaidi ya makadirio ya awali ya **Sh. 2,407,569,050.81**.

Mheshimiwa Spika, hadi taarifa hii inawasilishwa Bungeni, bado haijathibitishwa kupatikana kwa mkandarasi atakayekamilisha mradi huu. Mradi huu kuendelea kutelekezwa kunaendelea kuzorotesha miundombinu iliyopo.

2.3.7.4 Uendeshaji Usioridhisha wa Kiwanja cha Mpira cha Tanzanite Kwaraa

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia hesabu zilizokaguliwa, Kamati imebaini udhaifu katika mifumo ya uendeshaji na usimamizi wa Uwanja wa Tanzanite Kwaraa ambapo, Serikali kupitia Halmashauri ya Mji Babati ilifanya uwekezaji wenye thamani ya **Sh. Bilioni 2.5** katika Kiwanja hicho. Ili kuboresha utendaji wa uwanja huo, Tarehe 29 Julai 2024, Halmashauri iliingia makubaliano (*Memorandum of understanding*) na Kilabu cha soka Fountain Gate.

Kifungu cha 4.1(b–c) cha Hati ya makubaliano (MoU) kinaitaka Halmashauri kuhakikisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kukamilisha kazi za miundombinu, pamoja na kulipia gharama za umeme na maji yanayotumika katika matengenezo ya uwanja. Aidha, Kifungu cha 4.2(a–b) cha Hati ya Makubaliano kinaitaka Fountain Gate FC kutunza uwanja kwa gharama zake yenyewe, pamoja na kusaidia maendeleo na matengenezo ya uwanja wa michezo.

Mheshimiwa Spika, kinyume na Kanuni ya 97(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za mwaka 2024, mapungufu kadhaa yamebainika katika uendeshaji wa kichanja hicho. Mapungufu yaliyobainika ni katika maeneo ya kiutawala, matengenezo na uwajibikaji kifedha.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, ufanisi wa uwekezaji huo ni mdogo kutokana na ukweli kwamba, licha ya Serikali kuwekeza jumla ya **Sh. Bilioni 2.5**, mapato yatokanayo na uwanja huo ni **Milioni 29.27**. Mapato hayo ni **Asilimia 1.17** tu ya uwekezaji (ROI) na muda wa kurejesha gharama za uwekezaji utafikia takriban **miaka 85**.

Pamoja na ufanisi mdogo wa uwekezaji na usimamizi, changamoto nyingine zilizobainika ni kutokuwepo kwa mpango mahususi wa ukarabati na matengenezo ya uwanja, kutowekwa wazi kwa mchango wa Fountain Gate FC katika matengenezo, kutokuwepo kwa Sera ya uwekezaji na uendelevu wa uwanja kulikopelekea gharama za matengenezo na uendeshaji kuzidi mapato yatokanayo na uwanja, miundombinu ya uwanja isiyokamilika na ukosefu wa huduma muhimu.

Mheshimiwa Spika, mapungufu hayo yanatokana na pande zote mbili (Halmashauri na Fountain Gate FC) kutotekeleza wajibu wao kikamilifu kwa mujibu wa Hati ya Makubaliano (MoU) pamoja na Hati hiyo kutokuwa na ufafanuzi wa kutosha kuhusu masuala ya fedha na miongozo ya uendeshaji. Uwepo wa changamoto hizo unaweza

kusababisha upotefu wa fedha za umma na uharibifu wa miundombinu ya uwanja huo.

Mheshimiwa Spika, Afisa Masuuli aliieleza Kamati kuwa, Hati ya Makubaliano iliyopo kati ya Halmashauri na Fountain Gate FC itafanyiwa marekebisho ili kujumuisha masharti ya wazi ya kifedha, ikiwemo kiasi cha michango, uwiano wa mgawanyo wa gharama na muda wa utekelezaji, kwa kuzingatia matakwa ya TPLB. Kamati imemtaka Mkurugenzi kuhakikisha mapungufu yote yaliyobainika yanaondolewa haraka ili kuongeza ufanisi katika usimamizi na uwekezaji wa kiwanja hiko.

2.3.7.5 Uwekezaji usio na tija katika kampuni ya jengo la biashara la Jiji la Mwanza (Rock City Mall)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ni wanahisa katika Kampuni ya jengo la biashara la Jiji la Mwanza (Rock City Mall) kwa umiliki wa Hisa **Asilimia 6** na **Asilimia 4** mtawalia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa H/Jiji Mwanza, hisa zinazomilikiwa zina thamani ya **Bilioni 4.8** ikijumuisha ardhi ya Halmashauri yenye thamani ya **Bilioni 3.7**. Licha ya Kampuni kurekodi faida ya **Sh. 233.86** kwa mwaka 2022/23 na **Sh. Bilioni 1.1** kwa Mwaka 2023/24, Halmashauri haikupata gawio (Dividend) la uwekezaji wake kinyume na Kifungu cha 105 cha Hati ya uanzishwaji wa Kampuni (Memorandum of Association) iliyosainiwa Tarehe 10 Machi, 2010.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya uwekezaji katika jengo la biashara la Jiji la Mwanza ipo pia katika H/M Ilemela ambayo ina umiliki wa **Asilimia 4** wenye thamani ya **Sh. Bilioni 3.2**. Kama ilivyo katika H/Jiji la Mwanza, H/M ya Ilemela pia haikupata gawio katika kipindi chote cha uwekezaji. Hata hivyo, Halmashauri imetakiwa kulipa **Sh 732,960,000** ili kukamilisha mchango wake wa Bilioni 3.2.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi chote cha uwekezaji na kwa Halmashauri zote mbili, thamani ya hisa za Kampuni imeendelea kubaki bila mabadiliko katika kiasi cha **Sh. 100,000** kwa hisa moja tangu mwaka 2017 wala tathmini mpya ya ardhi haijafanyika. Kamati imeelezwa kuwa, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Halmashauri zinatarajia kupokea gawio la uwekezaji huo kwa **Sh. 27,586,000.20**.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano ya kina, Kamati haikuridhishwa na hali ya sasa ya uwekezaji pamoja na udhaifu wa Halmashauri katika kusimamia haki zao ili kupata gawio ambalo halikulipwa. Kamati haioni tija ya uwekezaji wa Halmashauri katika Kampuni hii endapo urekebishaji wa umiliki na mgawanyo mpya wa hisa hautazinufaisha Halmashauri husika.

2.3.8 Usimamizi Usioridhisha wa Rasilimali watu

Mheshimiwa Spika, Ili kuhakikisha Sheria na Kanuni zinazosimamia matumizi ya fedha za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zinasimamiwa ipasavyo, Kamati imeangalia pia eneo la rasilimali watu ambao ndio watekelezaji wakuu wa Sheria na Kanuni hizo. Katika

eneo hili, mambo yaliyoangaliwa ni ustawi wa watumishi na uhusiano kazini (Employee Welfare), masuala ya nidhamu na maadili, mafunzo, maendeleo na upandishwaji vyeo na usimamizi wa utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, mambo ya msingi yaliyojadiliwa na Kamati katika eneo hili ni kama ifuatavyo:-

2.3.8.1 Changamoto za Kiutendaji katika Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha ukaguzi wa ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kina jukumu la kisheria la kutoa huduma za ushauri na uhakiki huru kwa Afisa Masuuli (Mkurugenzi) ili kuhakikisha rasilimali za umma zinasimamiwa kwa uadilifu, ufanisi, na kwa kuzingatia Sheria. Sheria ya Fedha za Umma na Kanuni zake za Mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2024), pamoja na Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeelezea maudhui na utendaji wa kitengo hiki.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikiangalia nafasi ya Kitengo cha Ukaguzi wa ndani katika kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi ya fedha za umma katika Halmashauri zote nchini. Aidha, Kamati imebaini mapungufu ya kiutendaji ya Kitengo hicho yanayosababishwa na uhaba wa rasilimali fedha na vitendeakazi unaotokana na kutengwewa bajeti ndogo na kutotolewa kwa bajeti yote iliyoidhinishwa kwa ajili ya kitengo hiki hali inayozuia uwezo wa wakaguzi kuyafikia maeneo yote ya Halmashauri.

Sababu nyingine inayopunguza ufanisi wa kitengo hiki ni kuingiliwa kwa uhuru wa kiutendaji pamoja na uhaba wa wakaguzi wa ndani wenye taaluma maalum kwa ajili ya ukaguzi wa mifumo ya IT au uhandisi, jambo linalofanya ukaguzi wa mifumo ya kompyuta au miradi mikubwa ya ujenzi kuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, mfano wa baadhi ya Halmashauri zenye changamoto katika Kitengo cha ukaguzi wa ndani ni H/W Hanang' ambayo ina upungufu wa wakaguzi wa ndani (wakaguzi watatu badala ya watano walioidhinishwa katika ikama) na kutokuwepo kwa programu za mafunzo kuhusu mifumo ya uendeshaji kama vile HPMIS, TAUSI, MUSE, PLANREP, NEST na FFARS.

Mfano mwingine wa changamoto hii ni kutofanya kazi kikamilifu kwa Kitengo cha ukaguzi wa ndani katika H/W Geita kutokana na kitengo hiko kushindwa kufanya ukaguzi katika miradi ya maendeleo pamoja na kushindwa kufanya mapitio ya uandaaji na utekelezaji wa bajeti kulikosababishwa na upungufu wa wakaguzi na uhaba wa rasilimali fedha. Vile vile, H/Mji Kasulu ina Mkaguzi wa ndani mmoja tu, uhaba wa rasilimali fedha na kutokuwepo kwa mafunzo ya mifumo hali inayokwamisha utendaji kazi wa kitengo hiko.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri kutoviwezesha vitengo vya ukaguzi wa ndani kunapunguza ufanisi wa ukaguzi, kunadhoofisha mifumo ya udhibiti wa ndani, kuongeza vihatarishi vya matumizi mabaya ya fedha za umma na kuongeza ukikukwaji wa Sheria na Kanuni katika utendaji wa jumla wa Halmashauri. Kamati inazitaka

Halmashauri kuviboresha vitengo vya ukaguzi wa ndani kuwa na ikama inayojitosheleza na kuwapa mafunzo stahiki.

2.3.8.2 Halmashauri kuwa na wakuu wa Idara na Vitengo wasio na Sifa na Wanaokaimu kwa muda mrefu

Mheshimiwa Spika, uwepo wa wakuu wa Idara na vitengo wasio na sifa na wanaokaimu kwa muda mrefu ni moja ya changamoto ya utawala bora ambayo hujitokeza mara kwa mara katika ripoti za CAG. Hali hii inasababisha ufanisi duni katika usimamizi wa miradi ya maendeleo, matumizi mabaya ya rasilimali za umma na ukiukwaji wa Sheria za Utumishi wa Umma.

Katika Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati, Asilimia 90 zina wakuu wa Idara na Vitengo wanaokaimu kwa muda mrefu (zaidi ya miezi sita) kinyume na Sheria. Katika uchambuzi wake, sababu zilizoainishwa za kutokuwepo kwa wakuu wa Idara na vitengo kamili ni kuchelewa kukamilika kwa mchakato wa upekuzi na uhaba wa rasilimali watu wenye sifa.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa wakuu wa idara wasio na sifa na wanaokaimu kwa Muda Mrefu kunaathiri utendaji wa jumla wa Halmashauri kwa kushusha thamani ya fedha hasa katika utekelezaji wa miradi kutokana na watumishi wasio na sifa kushindwa kufanya tathmini ya kina ya miradi ya maendeleo kutokana na kutojiamini na hivyo kusababisha upotevu wa fedha za umma, kuongezeka kwa makosa ya kiutawala na kifedha kunakosababisha ongezeko la hoja za CAG na kushuka kwa morali ya kazi.

Katika majadiliano na Maafisa Masuuli, Halmashauri zilizobainika kuwa na wakuu wa Idara na vitengo wanaokaimu (zaidi ya watumishi Watano) ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 16: Idadi ya Wakuu wa Idara na Vitengo wanaokaimu kwa muda mrefu

S/N	Jina la Halmashauri	Idadi ya Wakuu wa Idara/Vitengo wanaokaimu
1.	H/W Moshi	12
2.	H/W Uvinza	10
3.	H/Mji Kasuli	9
4.	H/W Ruangwa	8
5.	H/W Bukombe	8
6.	H/Mji Njombe	8
7.	H/W Kasulu	8
6.	H/W Same	7
7.	H/W Bagamoyo	7
8.	H/W Hanang’	6
9.	H/Mji Babati	6
11.	H/M Ubungo	6
12.	H/W Kibaha	5 hawana sifa, 6 wanakaimu

Mheshimiwa Spika, uwepo wa idadi kubwa ya wakuu wa Idara na vitengo wanaokaimu kwa muda mrefu kunahatarisha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Halmashauri hasa katika usimamizi wa fedha za umma. Serikali (Ofisi ya Raisi Menejimenti ya

Utumisi wa Umma na Utawala Bora) inashauriwa kuchukua hatua za haraka ili kuondoa changamoto iliyopo.

2.3.8.3 Michango ya watumishi kutowasilishwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF)

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Halmashauri kukata na kuwasilisha michango ya watumishi kwa wakati kila mwezi katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, 2018 na miongozo ya Serikali. Hata hivyo, baadhi ya Maafisa Masuuli wamekuwa wamekiuka Kifungu cha 18(1) cha Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, baadhi ya Halmashauri zimeshindwa kupeleka michango ya watumishi kutokana na kutumia fedha za michango kwa shughuli nyingine badala ya kuziwasilisha katika mfuko, na kukosekana kwa uwajibikaji wa baadhi ya watendaji wa Halmashauri.

Pamoja na Kamati kusisitiza umuhimu wa michango ya watumishi kuwasilishwa kwa wakati, Changamoto hii imekuwa ikiongezeka kutoka **Sh. 2,633,819,855** zilizoripotiwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 hadi kufikia **Sh. Bilioni 3.90** katika mwaka wa fedha 2024/2025. Halmashauri ambazo hazikupeleka michango ya watumishi katika Mfuko kwa wakati na nyingine kutakiwa kulipa faini na adhabu ni kama inavyooneka katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 17: Halmashauri ambazo Hazikuwasilisha michango ya Watumishi katika Mfuko wa PSSSF

S/N	Jina la Halmashauri	Kiasi ambacho hakikupelekwa	Faini/Adhabu
1.	H/W Hanang’	Sh. 216,595,632.00	Sh. 225,954,247.00
2.	H/Mji Babati	Sh. 51,270,838.00	Sh. 65,754,8823.00
3.	H/W Bariadi	Sh. 180,723,885.00	Sh. 93,566,313.49
4.	H/W Mbeya	Sh. 197,313,414.00	-
5.	H/W Ruangwa	Sh. 63,712,098.00	-
6.	H/M Mtwara	Sh. 33,829,038.00	Sh. 262,629,883.00

Mheshimiwa Spika, Halmashauri kutowasilisha michango ya wananchi kunaongeza gharama kwa Halmashauri kutokana na kutakiwa kulipa faini/adhabu na mtumishi aliyefika ukomo wa utumishi wake (kustaafu) kuchelewa au kutolipwa kwa mafao yao ya mkupuo au pensheni ya kila mwezi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati inazitaka Halmashauri zote kuweka kipaumbele katika upelekaji wa michango ya watumishi ili kuimarisha ustawi wa wananchi hao.

2.3.9 Kukosekana kwa Udhibiti katika Usimamizi wa Mali za Umma

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka Kanuni za Usimamizi wa Mali za Umma za mwaka 2024 chini ya Sheria ya Fedha za Umma (Sura ya 348) ili kuleta uwajibikaji, ufanisi, na tija katika matumizi ya

rasilimali za umma ikijumuisha mali zilizopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kamati imeangalia kwa kina eneo hili ili kuhakikisha kunakuwa na mifumo thabiti ya upatikanaji, utunzaji, utumiaji, na ulinzi wa mali zote za umma zinazomilikiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Maeneo yaliyobainika kuwa na mapungufu ni kama ifiatavyo:-

2.3.9.1 Kutokuwepo kwa Matumizi Sahihi ya Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha imeanzisha mfumo wa kielektroniki wa GAMIS kwa ajili ya kusajili, kutunza, kuchakata na kuangalia taarifa za mali zote za taasisi za umma kama ilivyofafanuliwa katika Kanuni ya 4(1) ya Kanuni za Fedha za Umma na Usimamizi wa Mali za Umma, 2024. Licha ya kuwepo kwa Kanuni hiyo, ukaguzi wa CAG umebaini Maafisa Masuuli kutotumia mfumo wa GAMIS kwa usahihi kutokana na tofauti kati ya mali zilizosajiliwa katika mfumo na mali zilizopo (*physicallly*).

Maafisa Masuuli kushindwa kutumia mfumo huu kunasababishwa na watendaji wao kushindwa kuwajibika ipasavyo kwa kuchelewa kuingiza taarifa za ununuzi mpya na mabadiliko ya hali za mali (kuhuisha taarifa), Baadhi ya watendaji kufanya kazi kwa mazoea na kutumia taratibu za zamani za kurekodi mali kwenye madaftari (ledgers) badala ya kuingiza taarifa kidijitali kwa wakati, changamoto za miundombinu ya TEHAMA na uelewa mdogo na uhaba wa mafunzo ya kutosha ya mfumo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nyingi nchini zina changamoto ya kutoingiza mali zake kwa usahihi katika mfumo wa GAMIS. Aidha,

mfano wa Halmashauri hizo ambazo zimebainika kutotumia mfumo wa huo kikamilifu na mali zote za Halmashauri kutosajiliwa kwenye mfumo ni H/W Bariadi (mali za **Sh. 47,493,463,828**), H/W Busega (Mali za **Sh. 114,943,140**), H/M Bukoba (Mali za **Sh. 1,873,684,576.98**),

Mheshimiwa Spika, Kutowiana kwa taarifa za mali zilizopo na zile zilizosajiliwa kwenye mfumo husababisha upotevu wa mali za umma, Halmashauri kushindwa kufunga hesabu za mwaka kwa usahihi, kutokuwa na taarifa sahihi za kifedha kwakuwa, Mfumo wa GAMIS umeunganishwa na mifumo mingine ya Serikali kama vile mfumo wa malipo wa Serikali (GePG) na kukosekana kwa Kanzi-Data sahihi ya mali Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zimeieleza Kamati kuwa, zinaendelea na mchakato wa kukamilisha kuhakiki mali na kuhuisha daftari la mali ili taarifa za fedha ziweze kusomana na daftari la mali. Hata hivyo, Kamati hairidhishwi na kasi ya zoezi hilo kwakuwa, muda wa mwisho uliowekwa na Serikali wa miaka minne kwa ajili ya zoezi hilo umekwishakamilika. Kamati inazitaka Halmashauri zote kuwa na matumizi sahihi ya mfumo ili Serikali kuu iweze kutambua kiasi, idadi, na thamani halisi ya mali inazomiliki nchi nzima kwa ajili ya kupanga bajeti na mipango ya maendeleo.

2.3.9.2 Kukosekana kwa Mpango Rasmi wa Matengenezo na Uondoshaji wa Mali Chakavu

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mwongozo wa kutambua na kuondoa kwa wakati mali ambazo ni chakavu au zilizopoteza muda wa matumizi ili kupunguza hasara na uharibifu wa mali. Aidha, kila Halmashauri inatakiwa kuwa na mpango rasmi wa matengenezo ya mali za umma na mpango wa uondoshaji wa mali hizo yakiwemo magari chakavu kama ilivyotamkwa katika Kanuni ya 7(1) ya Kanuni za Fedha za Umma za Usimamizi wa Mali za Umma, 2024.

Uchambuzi wa Kamati katika eneo hili umebaini baadhi ya Halmashauri kutokuwa na mipango ya matengenezo ya mali. Sababu za changamoto hii ni pamoja na eneo la matengenezo kutokupewa kipaumbele wakati wa maandalizi ya bajeti na urasimu katika michakato ya Kisheria na ukaguzi ya uondoaji wa mali chakavu hasa kwa upande wa magari chakavu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 **magari 319** ambayo hayawezi kutengenezeka na hayahitajiki tena kwa utoaji wa huduma yameendelea kukaa katika Halmashauri bila kutumika kwa zaidi ya miezi 12 bila kuuzwa wala kuripotiwa kwa Katibu Mkuu, kinyume na Sheria. Mfano wa Halmashauri hizo ni H/Mji Babati magari Matano, H/W Hanang' magari Saba, H/W Liwale magari Matano, H/W Moshi magari Kumi na Sita na H/M Singida magari Sita.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Masuuli wameeleza juu ya mipango yao ya kufanya ukarabati wa mali chakavu na wengine kudai Hazina kuchelwa kutoa kibali cha uondoshaji wa magari hayo chakavu.

Kutozingatiwa kwa Kanuni ya 7(1) kunaisababishia Serikali kuingia gharama kubwa sana kununua vipuli vya bei ghali kwa ajili ya magari yaliyochoka badala ya kununua vyombo vipya, uharibifu wa mazingira na afya na kukwama kwa huduma za jamii. Kamati inasisitiza uzingatiaji wa Kanuni za utunzaji na uondoaji wa mali za umma.

2.3.10 Changamoto katika Usimamizi wa Ardhi

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za mitaa kwa kushirikiana na Ofisi ya Kamishna wa Ardhi wa Kanda, zimepewa dhamana ya kusimamia, kupanga, na kuratibu matumizi endelevu ya ardhi kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi (Sura 113) na Sheria ya Ardhi ya Vijiji (Sura 114). Majukumu yanayopaswa kutekelezwa na Halmashauri ni pamoja na upangaji na upimaji wa miji, utoaji wa hati miliki na leseni za makazi, utatuzi wa migogoro ya ardhi na kukusanya kodi ya ardhi.

Kinyume na matakwa ya Sheria na Kanuni, Kamati imebaini mapungufu mbalimbali katika usimamizi wa ardhi kama ifuatavyo:-

2.3.10.1 Kutozingatiwa kwa Taratibu za Uuzaji na Ugawaji wa Viwanja katika Manispaa ya Kibaha

Mheshimiwa Spika, Serikali chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI imeweka utaratibu wa uuzaji wa viwanja vya Halmashauri ili kuongeza uwazi na uwajibikaji pamoja na kuongeza mapato ya Halmashauri. Mfumo wa TAUSI umeanzishwa ili kuhakikisha mchakato mzima unakuwa ni wenye ufanisi.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ukaguzi wake katika Halmashauri ya Manispaa ya Kibaha, CAG alibaini mapungufu katika mauzo ya **viwanja 168** vyenye thamani ya **Sh. 4,091,838,000** ambayo yaliyofanyika nje ya mfumo wa TAUSI kinyume na taratibu. Licha ya mauzo hayo kufanyika nje ya mfumo, mkaguzi hakuweza kuthibithisha iwapo mapato ya **Sh. 3,610,065,500** yaliyotokana na mauzo hayo yalipokelewa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, licha ya kutotumia mfumo wa TAUSI katika mauzo ya viwanja tajwa hapo juu, Halmashauri haikuwa na mfumo thabiti wa udhibiti wa mapato ya ardhi kwakuwa, mchakato wa uuzaji wa viwanja haukufuata taratibu zilizowekwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kutozingatiwa kwa taratibu kumeifanya Halmashauri kupoteza jumla ya **Sh. 7,845,412,000** inayotokana na kugawa **viwanja 189** bila ya kupokea malipo ya mauzo ya viwanja hivyo.

Mheshimiwa Spika, kutokusanywa kwa kiasi hiko cha pesa kinapunguza mapato ya Halmashauri kwa kiasi kikubwa na kuashiria upotevu wa fedha za umma. Kamati imemtaka Afisa Masuuli kuhakikisha dosari zote zilizojitokeza katika uuzwaji wa viwanja zinaondolewa ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Afisa Masuuli aliieleza Kamati kuwa, baada ya hoja ya CAG, Halmashauri ilihakikisha viwanja vilivyohojiwa vinaingizwa katika mfumo wa TAUSI na wanufaika wote wameshaandikiwa barua na wamepewa muda wa miezi Sita ili waweze kulipa. Aidha, kwa watakaoshindwa kulipia viwanja hivyo,

taratibu nyingine zitafuatwa ikiwa ni pamoja na kuvirudisha viwanja hivyo na kuviuza kwa watu wengine.

2.3.10.2 Mali za Halmashauri kukosa Hati Miliki na Maeneo ya Wazi kukosa Usimamizi

Mheshimiwa Spika, Kukosekana kwa hati miliki kwenye ardhi na mali za Halmashauri ni changamoto kubwa inayozikabili Halmashaiuri nyingi. Licha ya Katibu Mkuu na Msajili wa Hazina kutuma barua zenye kumbukumbu Na. CAB142/626/01/A/42 ya tarehe 26 Septemba, 2014 na CNA.32/572/01/96 mtawalia, wakielekeza upatikanaji wa vyeti vya Hati ya Umiliki kwa viwanja vinavyomilikiwa na Serikali.

Hata hivyo, bado kuna Halmashauri ambazo zina miradi na majengo katika viwanja ambavyo havina hati za umiliki kinyume na matakwa Sheria, Kanuni na Miongozo. Aidha, vifungu vya 7(5)(s) na 28(f) vya Sheria ya Mipango Miji, Sura ya 355 vinazitaka Halmashauri kutunza maeneo yake ya wazi.

Kuchelewa kwa michakato ya upimaji ardhi, uthamini, na uandaaji wa hati miliki za Halmashauri kunasababishwa na urasimu na ucheleweshaji, usimamizi dhaifu wa mali za Umma na ufuatiliaji duni wa menejimenti ya Halmashauri katika kuchakata nyaraka za umiliki kabla ya kuanza miradi ya ujenzi. Baadhi ya Halmashauri ambazo zina maeneo mengi yasiyo na hati miliki ni H/W Moshi **maeneo 476**, H/W Namtumbo **maeneo 102**, H/M Kigamboni **Viwanja vya wazi 89** na H/Jiji Mbeya kuwa na maeneo 68 yasiyoendelezwa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri kukosa hati za umiliki katika maeneo yake kunaweza kusababisha uvamizi wa ardhi hasa maeneo ya wazi, viwanja vya shule, masoko, na hospitali kutokana na kukosekana kwa nyaraka za kisheria zinazolinda maeneo hayo hali inapelekea migogoro ya ardhi baina ya Halmashauri na wananchi. Athari nyingine ni Halmashauri kushindwa kukodisha au kuuza maeneo yake kwa wawekezaji kwa thamani halisi ya soko kutokana na maeneo hayo kukosa hati za umiliki.

Mheshimiwa Spika, Kamati inazishauri Halmashauri zote kutenga bajeti maalumu kila mwaka kwa ajili ya uratibu na upimaji wa maeneo yao, pamoja na kutumia mifumo ya kidijitali kulinda na kusajili mali zote za umma pamoja na kuwa matumizi bora ya maeneo yote ya wazi yanayomilikiwa na Halmashauri.

2.3.10.3 Usimamizi wa Ardhi Usioridhisha katika H/Jiji la Tanga

Mheshimiwa Spika, Halmashauri kupitia Idara ya Ardhi zinapaswa kuchukua hatua za kisheria na kiutawala ili kubaini maeneo yote yanayomilikiwa na Halmashauri. Mchakato huo huusisha michoro ya mipango miji, ramani za upimaji, uwekaji wa alama sahihi na kuingiza katika mfumo wa Serikali viwanja vilivyotambuliwa na kupimwa.

Kinyume na taratibu hizo, Katika miaka ya fedha 2018/19 hadi 2021/22, Halmashauri ilipima **viwanja 3,782** vya Kange Kasera na Mkurumuzi vyenye thamani ya **Sh. 3,477,022,405** kwa ajili ya kurasimisha umiliki wa maeneo ya Serikali yaliyovamiwa. Hata hivyo, Halmashauri ilishindwa kuwatambua wamiliki wenye **viwanja 2,268**

vyenye thamani ya **Sh. 2,562,807,115** na kusababisha mapato hayo kutokusanywa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Afisa Masuuli alieeleza Kamati kuwa, wakati wa zoezi la urasimishaji, wamiliki wa maeneo hayo hawakushiriki katika mchakato wa urasimishaji na uhalalishaji wa umiliki wa maeneo yao. Tofauti na maelezo hayo, katika kipindi cha ukaguzi, CAG alifanya uhakiki wa **viwanja 20** na kubaini **viwanja 11** vilikwishaendelezwa.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati baada ya majibu ya Menejimenti na Ripoti ya CAG umebaini kuwa, Halmashauri haikutekeleza majukumu yake kikamilifu katika kuhakikisha wamiliki wote wanatambulika na fedha zote zinakusanywa. Vile vile, kwa upande wa viwanja ambavyo wamiliki wake wametambuliwa, Halmashauri ilishindwa kukusanya jumla ya **Sh. 914,215,290** sawa na **Asilimia 59** ya kiasi kilichopaswa kukusanya.

Mheshimiwa Spika, udhaifu katika uuzaji wa viwanja ulitokea pia katika maeneo ya Amboni ambapo, Halmashauri iliuza viwanja 758 katika eneo hilo vyenye thamani ya **Sh. 4,650,339,000** bila kuingiza viwanja hivyo katika Mfumo wa TAUSI. Aidha, hakuna Ushahidi wa malipo hayo ikijumuisha ada za maombi. Vile vile, viwanja vinne katika eneo la viwanda la Pongwe vyenye thamani ya **Sh. 222,385,000** viliuzwa bila ya kuingizwa katika Mfumo wa TAUSI.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeitaka Halmashauri ya Jiji la Tanga pamoja na Halmashauri zote nchini kuhakikiwa wanakuwa na mifumo

Thabiti ya ufuatiliaji wa mapato ya ardhi ili mapato yote ya Halmashauri yaweze kukusanywa.

2.3.10.4 Fidia ya Ardhi Isiyolipwa kwa Wakati Sh. Bilioni 28.76

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ardhi na Sheria za Uthamini zinazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kulipa fidia ya ardhi kwa wananchi kabla ya kutwaa maeneo yao ili kufidia thamani ya uwekezaji na maendeleo pamoja na kuzuia migogoro ya ardhi. Hata hivyo kuna Halmashauri ambazo hazijalipa madai yake ya fidia kinyume na Kifungu cha 11(1) cha Sheria ya Utwaaji wa Ardhi, Sura ya 118.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati kwa hoja zilizowasilishwa mbele yake umebaini sababu mbalimbali zinazosababisha Halmashauri kutolipa fidia kwa wananchi kwa wakati ambazo ni kutoandaa bajeti ya ulipaji wa fidia kabla ya kuanza kwa zoezi la uchukuaji wa maeneo, mivutano ya kisheria juu ya tathimini ya maeneo yaliyotwaliwa na wananchi kukosa nyaraka halali za umiliki wa maeneo yao.

Tatizo la Halmashauri kutolipa fidia limekuwa likijirudia kila mwaka. Katika Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati, Halmashauri ambazo hazijalipa madai ya fidia kwa wananchi wake ni pamoja na H/Mji Babati **Sh. 347,460,799**, H/M Shinyanga **Sh. 65,074,223.50**, H/Jiji Mwanza **Sh. 4,248,194,021**, H/M Ilemela **Sh. 3,347,455,625**, H/Jiji Mbeya **Sh. 1,011,550,219**, na H/M Mtwara **Sh. 438,005,781**.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri kutwaa maeneo ya wananchi bila ya kulipa fidia kwa muda uliopangwa kisheria kunaweza kusababisha kuongezeka kwa migogoro ya ardhi, kukwama au kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ongezeko la madeni na riba na kuongezeka kwa gharama za kesi endapo mashauri yatafunguliwa. Ili kuzuia Athari hizo, Kamati inazishauri Halmashauri zote kulipa haki na stahiki za wananchi kabla ya kutwaa maeneo yao.

2.3.11 Utekelezaji usioridhisha wa Mapendekezo ya Kamati na Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 14 (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025 inaitaka Kamati kufuatilia utekelezaji wa Mapendendezo ya Kamati yaliyotolewa chini ya Kifungu cha 14 (c) ya Nyongeza ya Nane. Vile vile, baada ya kukamilika kwa mchakato wa ukaguzi, CAG hutoa hoja kwa Halmashauri husika. Katika eneo hili, mambo mahususi yaliyoangaliwa ni yafuatayo:-

2.3.11.1 Utekelezaji Usioridhisha wa Mapendekezo ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kila Kamati inapomaliza mahojiano na Maafisa Masuuli, hutoa mapendekezo ambayo Halmashauri hupaswa kuyatekeleza ndani ya muda ulipangwa na Kamati. Halmashauri inaporudi tena mbele ya Kamati, jambo la kwanza ambalo Kamati huangalia ni iwapo mapendekezo yaliyotolewa katika kikao kilichopita yametekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhishwa na mwenendo wa utekelezaji wa Mapendekezo yake hivyo kuzitaka Halmashauri zote kuhakikisha wanatekeleza mapendekezo yote kikamilifu. Kutoridhishwa kwa mwenendo wa utekelezaji kunatokana na ukweli kwamba, katika mwaka 2024/2025, ni **Asilimia 29.2** pekee ya Mapendekezo yote **1,176** ndiyo yaliyotekelezwa kikamilifu. Aidha, **Asilimia 60.3** yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na yaliyosalia utekelezaji wake haujaanza kabisa.

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mapendekezo yaliyotekelezwa kikamilifu ni **Asilimia 23.2** tu ya Mapendekezo yote **1,212**. Aidha, **Asilimia 56.6** yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na yaliyosalia hayajatekelezwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi wa hesabu zilizokaguliwa, Halmashauri ambazo hazikutekeleza kikamilifu mapendekezo ya Kamati ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 18: **Halmashauri ambazo hazijatekeleza kikamilifu mapendekezo ya Kamati**

Jina la Halmashauri	**Mapendekezo yaliyotolewa**	**Mapendekezo yaliyotekelezwa kikamilifu**	**Mapendekezo yasiyotekelezwa kikamilifu (yaliyo katika hatua mbalimbali)**
H/W Nachingwea	4	0	4
H/W Bagamoyo	6	0	6
H/W Same	7	2	5

H/W Msalala	5	1	4
H/W Bariadi	4	1	3

Mheshimiwa Spika, kamati inazitaka Halmashauri zote kuhakikisha zinatekelezwa kikamilifu mapendekezo yote ya Kamati kwa muda uliopangwa ili kuondoa mapungufu yaliyobainika.

2.3.11.2 Utekelezaji Usioridhisha wa Hoja na Mapendekezo ya CAG

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikufuatilia ni kwa namna gani na kwa kiasi gani Halmashauri zimekuwa zikitekeleza Mapendekezo yanayotolewa na CAG kwa kila mwaka. Zoezi hilo hufanyika ili kuhakikisha kazi inayotekelezwa na jicho la bunge kwa niaba yao inaleta tija na hoja zilizoibuliwa zinatekelezwa ili kupunguza matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za umma.

Kamati haijaridhishwa na utekelezaji wa Mapendekezo yaliyotolewa na CAG kwakuwa, Katika Mwaka wa fedha 2024/2025 ni **Asilimia 41** tu ya mapendekezo yote **14,433** ndizo zilizotekelezwa kikamilifu huku **Asilimia 56** utekelezaji wake haujakamilika kikamilifu na Asilimia **3** ya mapendekezo yamepitwa na wakati. Halmashauri ambazo hazijatekeleza Mapendekezo ya CAG kwa kiasi kikubwa ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 19: Halmashauri ambazo hazijatekeleza kikamilifu mapendekezo ya CAG kwa kiasi kikubwa

Jina la Halmashauri	**Mapendekezo yaliyotolewa**	**Mapendekezo yaliyotekelezwa kikamilifu**	**Mapendekezo yasiyotekelezwa kikamilifu (yaliyo katika hatua mbalimbali)**
H/W Same	18	4	14
H/W Msalala	39	7	32
H/Mji Babati	31	7	24
H/W Mbozi	10	3	7
H/W Geita	39	7	29

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya CAG kutotekelezwa kikamilifu kunaashiria kuendelea kwa matumizi mabaya ya fedha za umma. Kamati inazitaka Halmashauri kukamilisha utekelezaji wa mapendekezo yote ya CAG.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Melezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa na mahojiano na Maafisa Masuuli waliofika mbele ya Kamati, kamati ina Maoni na Mapendekezo kama ifuatavyo:-

3.2 Maoni

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua mbalimbali za kiutendaji zinazochukuliwa na Serikali katika kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za Umma, bado kuna changamoto katika uendeshaji wa Halmashauri nyingi. Kamati imebaini kuwa, hatua Madhubuti na za haraka za kiutendaji, kinidhamu na kisheria zinapaswa kuchukuliwa. Changamoto zilizobainika zipo katika maeneo yafuatayo: -

a) **Usimamizi usioridhisha katika Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri:** Baadhi ya Halmashauri zimeshindwa kukusanya mapato ya ndani ili kupata fedha ya kutosha kwa ajili ya uendeshaji bora wa Halmashauri na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Changamoto hii inapunguza juhudi za Serikali za kuleta maendeleo kwa jamii.

b) **Matumizi ya Fedha za Umma kinyume na Sheria na Kanuni pamoja na usimamizi usioridhisha wa Akaunti ya Amana**: Baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikifanya matumizi ya fedha za umma kinyume na matakwa ya Sheria, kanuni na Miongozo. Hali hii inaongeza uwezekano wa fedha za Umma kutumika katika maeneo yasiyopangwa pamoja na kusababisha upotevu wa fedha za umma.

c) **Ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na mapungufu katika usimamizi wa Mikataba**: Baadhi ya Halmashauri zimebainika kukiuka matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma kwa kutofanya tathmini sahihi ya zabuni na kushindwa kusimamia mikataba ipasavyo. Ukiukwaji wa Sheria hizo unachochea kuongezeka kwa gharama za huduma na miradi.

d) **Madeni ya Halmashauri kutolipwa kwa wakati (Payables):** Halmashauri nyingi zimekuwa na malimbikizo ya madeni ya watumishi na wazabuni ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu. Uwepo wa madeni hayo unaondoa dhana ya uwajibikaji katika Halmashauri hizo.

e) **Mapungufu katika utekelezaji wa miradi ya Maendeleo:** Utekelezaji wa miradi ni kipaumbele cha Serikali kwa wananchi wake. Hata hivyo Halmashauri zimekuwa zikishindwa kukamilisha miradi yake kwa wakati kunakotokana na fedha kutopatikana kwa wakati.

f) **Mapungufu katika Usimamizi wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu**: Baadhi ya Halmashauri hazizingatii matakwa ya Sheria na Kanuni za uendeshaji na usimamizi wa Mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kutowasilisha michango katika mfuko huo. Ukiukwaji wa Kanuni unakwamisha dhamira ya Serikali kuwasaidia wananchi wake.

g) **Kukosekana kwa mipango sahihi ya uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**: Baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikifanya uwekezaji bila ya kufanya upembuzi yakinifu juu ya faida itakayopatikana. Kuwepo kwa miradi isiyo na tija kunaongeza upotevu wa fedha za umma.

h) **Usimamizi Usioridhisha wa Rasilimali watu**: ukiukwaji wa utawala bora umekuwa ukifanyika katika baadhi ya Halmashauri kutokana na watumishi kutopata stahili zao kwa wakati na kukosekana kwa watumishi wenye sifa. Changamoto hii inazifanya Halmashauri kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

i) **Kukosekana kwa Udhibiti katika Usimamizi wa Mali za Umma**: Baadhi ya Halmashauri zimekuwa na usimamizi usioridhisha wa mali zake hali inayoweza kusababisha upotevu wa mali hizo na kukosekana kwa taarifa sahihi za mali za Halmashauri.

j) **Changamoto katika Usimamizi wa Ardhi**: usimamizi usioridhisha wa ardhi kwa kiasi kikubwa umechangia upotevu wa mapato ya Halmashauri na uvamizi wa viwanja. Hali hii inatokana na kukiukwa kwa taratibu za uuzaji na ugawaji wa viwanja katika maeneo mbalimbali.

3.3 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, utoaji wa mapendekezo ya Kamati ambayo yatakuwa ni Maazimio ya Bunge umezingatia hoja iliyopo, athari ya hoja hiyo pamoja na hatua zinazopaswa kuchukuliwa na Serikali ili kuondoa hoja hizo. Licha ya Hoja na Mapendekezo ya CAG kuendelea kujirudia kila mwaka, Kamati inatambua hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuhakikisha mapendekezo ya kamati na mapendekezo ya CAG yanatekelezwa kikamilifu.

Kwa muktadha wa uchambuzi wa Taarifa ya CAG kwa hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2025, Mapendekezo ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

3.3.1 Usimamizi Usioridhisha katika Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri

KWA KUWA, Halmashauri nyingi nchini zimekosa mikakati madhubuti ya kuongeza mapato ya ndani na kuendelea kutegemea ruzuku ya Serikali kwa kiasi kikubwa,

NA KWA KUWA, utegemezi wa ruzuku ya Serikali Kuu kwa kiasi kikubwa inaziweka Halmashauri katika hatari ya kushindwa

kujiendesha kwa ufanisi, kupunguza uhuru wa kifedha (kushindwa kumudu gharama za uendeshaji) na kuathiri utoaji wa huduma za kijamii kwa wananchi na kushindwa kuwekeza katika miradi ya kimkakati,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali ihakikishe Halmashauri zinakusanya mapato ya **Sh. Bilioni 8.52** yatokanayo na ushuru wa huduma kabla ya Tarehe 30 Disemba, 2027;

b) Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ilipe deni lake la **Sh. 2,916,960,362.00** kwa Halmashauri Saba zilizofika mbele ya Kamati sambamba na Halmashauri zote nchini zenye madai ya aina hiyo kabla ya Tarehe 30 Disemba, 2027;

c) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi izilipe Halmashauri **Sh. Bilioni 13.54** zinazotokana na marejesho ya Asilimia 20 ya Kodi ya Ardhi kabla ya Tarehe 30 Juni, 2028;

d) Serikali ihakikishe kabla ya Tarehe 30 Januari, 2027, Halmashauri zote ziwe zimehuisha kanzi data ya walipa kodi ili kupata taarifa na idadi sahihi ya wafanyabiashara wanaostahili kulipa ushuru wa huduma katika maeneo yao na taarifa hiyo iwasilishwe kwa CAG kabla ya Tarehe 30 Machi, 2027;

e) Ofisi za Wakuu wa Mikoa kupitia Makatibu Tawala wa Mikoa (RAS) katika mikoa yote zisimamie na kuhakikisha kuwa, uchunguzi wa mashauri yaliyopo TAKUKURU unakamilika

haraka na hatua za kisheria zichukuliwe kabla ya kukamilika kwa mwaka wa fedha 2027/2028

3.3.2 Matumizi ya Fedha za Umma Kinyume na Sheria na Kanuni pamoja na Usimamizi Usioridhisha wa Akaunti ya Amana

KWA KUWA, Kamati imebaini baadhi ya Halmashauri kufanya matumizi ya fedha za umma kinyume na Sheria na Kanuni,

NA KWA KUWA, Ukiukwaji wa Sheria hizo umesababisha matumizi mabaya ya fedha za umma,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali ihakikishe Halmashauri zinakusanya masurufu ya **Sh. 1,016,728,241** kabla ya Tarehe 30 Juni, 2027 kwa kuzingatia Sheria na Kanuni;

b) Serikali ihakikishe Halmashauri zinarejesha **Sh. 1,585,358,228** zilizoazimwa kutoka katika mfuko wa Amana kabla ya Tarehe 30 Juni, 2027;

3.3.3 Ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na Mapungufu katika Usimamizi wa Mikataba

KWA KUWA, Baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikikiuka matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na Kanuni zake katika utekelezaji wa majukumu yake,

NA KWA KUWA, ukiukwaji wa wa Sheria hizo umesababisha upotevu wa fedha za umma, kuongezeka kwa gharama za

mikataba na kukosekana kwa thamani ya fedha (value for money) katika ununuzi wa umma,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali ihakikishe kuwa, katika mwaka wa fedha 2026/2027, ununuzi wote wa umma ufanyike kupitia mfumo wa ununuzi wa kielekitroniki (NeST);

b) Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ifanye ukaguzi wa kina katika maeneo yote yenye dosari zilizoainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuchukua hatua stahiki;

c) Serikali ihakikishe Halmashauri ya Jiji la Dodoma inaondoa dosari zote za kimkataba zinazohusiana na upangishaji wa Hoteli ya Dodoma jiji kabla ya Tarehe 30 Disemba, 2027.

3.3.4 Madeni ya Halmashauri Kutolipwa kwa Wakati

KWA KUWA, Halmashauri nyingi zimekuwa na madeni ya watumishi na wazabuni ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu;

NA KWA KUWA, kutolipwa kwa madeni hayo kwa wakati kuna athari hasi za kiuchumi, kiutendaji na kijamii;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali (Wizara ya Fedha) ilipe madeni yote ya watumishi na wazabuni yaliyohojiwa na CAG kwa hesabu zinazoishia tarehe 30 Juni, 2025; na

b) Serikali ihakikishe Halmashauri zote zinatenga bajeti ya kutosha ya ulipaji wa madeni ya watumishi na wazabuni na madeni yote yaliyoainishwa katika ripoti ya CAG kwa hesabu zinazoishia Tarehe 30 Juni, 2025 yalipwe kulingana na umri wa madeni hayo.

3.3.5 Mapungufu katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

KWA KUWA, kumekuwepo kwa changamoto nyingi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama miradi kutokamilika kwa wakati na Halmashauri kutotenga fedha za mapato ya ndani (Asilimia 70, 60, 40 na 20) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

NA KWA KUWA, changamoto hizo zimesababisha wananchi kukosa faida na tija iliyotarajiwa kupatikana kutokana na utekelezwaji wa miradi katika maeneo yao;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali ihakikishe inatenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi yote ikiwa ni pamoja na miradi iliyotekelezwa kwa nguvu za wananchi pamoja na miradi ya kimkakati ya ujenzi wa Stendi ya Mabasi Ngangamfumuni Moshi, Wodi ya Upasuaji katika Hospitali ya Mji Tunduma, Ofisi za Idara ya Afya katika H/Jiji Mwanza na jengo la Makao Makuu ya Halmashauri ya Sikonge kabla ya Tarehe 30 Juni, 2029;

b) Serikali ihakikishe SUMA JKT inakamilisha miradi yake katika Halmashauri zote kwa kuzingatia matakwa ya mikataba iliyopo;

c) Serikali ihakikishe ifikapo Tarehe 30 Juni, 2029, Halmashauri ziwe zimepeleka fedha za miradi ya maendeleo **Sh. Bilioni 36.92** ambazo hazikutengwa kutoka katika mapato ya ndani katika mwaka wa fedha 2024/2025;

d) Serikali ifanye mapitio ya viwango vilivyowekwa vya uchangiaji wa mapato ya ndani katika miradi ya maendeleo ili kuwa na viwango vinavyoendana na uhalisia na uwezo wa kifedha wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Jukumu hilo litekelezwe kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha 2027/2028; na

e) Serikali ihakikishe Kampuni zote zinazomiliki leseni za madini zinatimiza wajibu wake kwa jamii kama ilivyoelekezwa katika Kanuni za wajibu wa wamiliki wa leseni za madini kwa jamii za Mwaka 2023.

3.3.6 Mapungufu katika Usimamizi wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu

KWA KUWA, Kamati imebaini mapungufu kadhaa katika uendeshaji na usimamizi wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu;

NA KWA KUWA, mapungufu hayo yanasababisha dhima ya Serikali ya kuwainua kiuchumi wananchi wake kupitia fedha za Mfuko huo kutofikiwa kwa kiasi kikubwa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali ihakikishe Halmashauri zinawasilisha **Sh. 13,882,521,799** ambazo ni Asilimia 10 kutoka katika mapato ya ndani kwenda katika Mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kabla ya Tarehe 30 Juni, 2028;

b) Serikali ihakikishe inachukua hatua stahiki na Halmashauri zinakusanya **Sh. Bilioni 120.48** zilizokopeshwa katika vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kabla ya Tarehe 30 Juni, 2028;

c) Serikali ihakikishe Halmashauri zinatoa mikopo kwa kuzingatia uwiano wa 4:4:2.

3.3.7 Kukosekana kwa Mipango Sahihi ya Uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

KWA KUWA, uwekezaji uliofanywa na baadhi ya Halmashauri katika miradi ya kimkakati kama stendi za mabasi, masoko ya kisasa na majengo ya vitegauchumi umekumbwa na changamoto nyingi za kiutendaji;

NA KWA KUWA, changamoto hizo zimesababisha miradi hiyo hiyo kutoleta faida iliyokusudiwa, kukosekana kwa thamani ya fedha (value for money), kukwamisha utoaji wa huduma stahiki kwa wananchi na kusababisha upotevu wa fedha za umma;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali ihakikishe inaongeza usimamizi na kuboresha miundombinu muhimu katika vituo vya mabasi na kuondoa dosari zote zilizobainishwa na CAG ili vituo hivyo viweze kutumika kikamilifu na mapato yaliyotarajiwa yaweze kukusanywa;

b) Serikali ihakikishe Kampuni ya jengo la biashara la Jiji la Mwanza (Rock City Mall) inazingatia Sheria na Kanuni ili Halmashauri ya Jiji Mwanza na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ziweze kupata gawio linalotokana na uwekezaji katika kampuni hiyo;

3.3.8 Usimamizi Usioridhisha wa Rasilimali Watu

KWA KUWA, mapungufu kadhaa yamebainika katika usimamizi wa rasilimali watu ikiwa ni pamoja na uwepo wa wakuu wa Idara na Vitengo wanaokaimu kwa muda mrefu, Kitengo cha ukaguzi wa ndani kutopewa rasilimali za kutosha na Michango ya watumishi kutowasilishwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF);

NA KWA KUWA, kutoondolewa kwa mapungufu hayo kunapunguza ufanisi, weledi na uwajibikaji wa watumishi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali ihakikishe Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani katika Halmashauri zote kinapatiwa rasilimali za kutosha (rasilimali

watu kwa mujibu wa ikama, rasilimali fedha na vitendea kazi) na Wakaguzi wa Ndani wapatiwe mafunzo kuhusu mifumo mbalimbali inayotumika katika Halmashauri;

b) Serikali ihakikishe Halmashauri zote zinakuwa na Wakuu wa Idara na Vitengo wanaokidhi vigezo vya kisheria na kiutendaji; na

c) Serikali ihakikishe Halmashauri zinawasilisha michango ya watumishi **Sh. Bilioni 3.90** katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) kabla ya tarehe 30 Disemba, 2027.

3.3.9 Kukosekana kwa Udhibiti katika Usimamizi wa Mali za Umma

KWA KUWA, Halmashauri nyingi zimebainika kutotumia kikamilifu mifumo thabiti ya upatikanaji, utunzaji, utumiaji, na ulinzi wa mali za umma zinazomilikiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

NA KWA KUWA, kutotumika ipasavyo kwa mifumo hiyo kunaweza kusababisha upotevu wa mali za umma, kutokuwa na taarifa sahihi za kifedha na kukosekana kwa Kanzi-Data sahihi ya mali kitaifa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali ihakikishe kabla ya Tarehe 30 Juni, 2027, Halmashauri zote ziwe zimeingiza mali zake zote kwa usahihi katika Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali GAMIS; na

b) Serikali ihakikishe kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha 2027/2028, Halmashauri zote ziwe zimefanya matengenezo na kuondoa mali chakavu kwa kuzingatia Kanuni ya 7(1) ya Kanuni za Fedha za Umma za Usimamizi wa Mali za Umma, 2024.

3.3.10 Changamoto katika Usimamizi wa Ardhi

KWA KUWA, kumebainika baadhi ya Halmashauri kukiuka matakwa ya Sheria ya Ardhi (Sura 113) na Sheria ya Ardhi ya Vijiji (Sura 114) pamoja na Miongozo ya Serikali inayohusu usimamizi wa Ardhi;

NA KWA KUWA, ukiukwaji wa Sheria na Miongozo hiyo umesababisha upotevu wa fedha zinazotokana na uuzwaji wa viwanja, uvamizi wa maeneo ya Halmashauri na wananchi kutolipwa fidia ya ardhi katika muda wa kisheria;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:

a) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) afanye Ukaguzi Maalumu katika Halmashauri ya Jiji la Tanga kwa miaka Mitatu (2022/2023, 2023/2024 na 2024/2025). Ukaguzi huo unalenga kubaini uzingatiaji wa masharti yanayotumika, kuthibitisha dosari na kiasi kinachohusika, kuchambua sababu na athari zake, na kupendekeza hatua za marekebisho na uwajibikaji kwa kuzingatia ushahidi. Aidha, Ukaguzi ufanyike kwa kuzingatia Hadidu za Rejea zifuatazo:-

    i. Ukusanyaji na uwasilishaji wa mapato ya ndani;

ii. Uuzaji wa viwanja 3,782 Kange Kasera na Mkurumuzi;

iii. Uuzaji wa viwanja 758 Amboni;

iv. Uuzaji wa viwanja vinne katika eneo la viwanda Pongwe;

v. Matumizi ya fedha za maendeleo kwa mwaka 2024/25;

vi. Ada na tozo za uchimbaji wa madini ya ujenzi; na

vii. Mapato ya stendi za Kange na Ngamiani na udhibiti wa ndani.

b) Serikali ihakikishe hadi kufikia tarehe 30 Disemba, 2027, Halmashauri zote zinakuwa na Hati Miliki za Ardhi za maeneo yao; na

c) Serikali ihakikishe inalipa Fidia ya Ardhi ya **Sh. Bilioni 28.76** kwa wananchi waliochukuliwa maeneo yao kwa mujibu wa Sheria.

3.3.11 Utekelezaji Usioridhisha wa mapendekezo ya Kamati na Hoja na Mapendekezo yote yaliyotolewa katika taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa

KWA KUWA, bado kuna hoja ambazo zimesababisha utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na CAG kwa Halmashauri zote nchini kutofanyika kikamilifu;

NA KWA KUWA, kutokamilika kwa utekelezaji wa mapendekeo ya CAG kunaashiria uendelevu wa matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Halmashauri zote;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itekeleze kikamilifu mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati pamoja na CAG katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka ya fedha ya 2023/2024 na 2024/2025.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

1.1 Hitimisho

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa dhati napenda kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri pamoja na kutoa miongozo na maelekezo yaliyoiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake kikamilifu bila ya vikwazo. Vile vile, napenda kumshukuru Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa uvumilivu wao wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii na kufanya kazi kwa ufanisi na weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Ado Shaibu Ado, Mb. - Mwenyekiti
2. Mhe. Abdallah Dadi Chikota, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Esther Amos Bulaya, Mb. - Mjumbe
4. Mhe. Joseph Enock Tama, Mb. - Mjumbe
5. Mhe. Salum Khamis Salim, Mb. - Mjumbe
6. Mhe. Emmanuel John Khambay, Mb. - Mjumbe
7. Mhe. Edibily Kazala Kinyoma, Mb. - Mjumbe

8. Mhe. Lutengano George Mwaliba, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Kiza Hussein Mayeye, Mb. - Mjumbe
10. Mhe. Amina Mussa Mkumba, Mb. - Mjumbe
11. Mhe. Faraji Buriani Nandala, Mb. - Mjumbe
12. Mhe. Naomy Duncan Mwaipopo, Mb. - Mjumbe
13. Mhe. Kinjekitile Ngombale Mwiru, Mb. - Mjumbe
14. Mhe. Josephine Joseph Kapoma, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Tunu Juma Kondo, Mb. - Mjumbe
16. Mhe. Charles Jacob Sungura, Mb. - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka I. Leonard kwa ushauri wake kwa Kamati pamoja na wasaidizi wake wote kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kusomwa kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho japo siyo kwa umuhimu, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) na kwa namna ya kipekee kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ndugu Charles Kichere. Aidha, napenda kuishukuru OWM – TAMISEMI ikiongozwa na Waziri Mhe. Riziki R. Shemdoe, Mb pamoja na Wizara ya Fedha kwa ushirikiano walioutoa katika Kamati kwa kutoa ufafanuzi kila ilipohitajika kufanya hivyo.

4.1 Hoja

Mheshimiwa Spika, Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa Hoja

Ado Shaibu Ado, Mb.

MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC)

03 Novemba, 2026

Kiambatisho Na. 1: Mchanganuo wa upokeaji wa ruzuku ya Serikali ikilinganishwana na ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa Halmashauri 75 zilizofika mbele ya Kamati.

S/N	Jina la Halmashauri	Fedha za Maendeleo	Asilimia	Fedha za OC	Asilimia	Mapato ya Ndani
1	BARIADI DC	10,371,571,544.00	122	26,629,010,781.00	108	2,538,141,915.00
2	BUSEGA DC	6,454,865,423.00	88	27,847,322,757.00	90	2,819,010,188.00
3	BUKOBA MC	11,655,370,238.00	79	24,342,222,203.00	103	3,711,041,874.00
4	KARAGWE DC	13,739,285,231.00	101.53	36,068,001,402.00	106	6,045,856,502.00
5	MISSENYI DC	9,098,948,173.00	68	25,395,236,958.00	103	11,841,564,512.00
6	KIGOMA MC	10,753,891,896.00	129	25,157,296,406.00	94	4,605,692,664.00
7	SUMBAWANGA MC	7,922,715,579.00	84	36,323,736,531.00	98	4,205,259,040.00
8	SIKONGE DC	32,264,042,681.00	99.6	24,485,811,162.00	105	4,880,141,135.00
9	GEITA DC	18,009,789,281.35	128.21	67,219,237,512.00	115.52	10,450,866,507.31
10	HANANG' DC	12,961,353,791.00	98	34,908,607,376.00	78	7,260,718,191.00
11	MSALALA DC	8,237,309,669.00	75	27,444,505,504.00	82	6,594,453,367.00
12	UBUNGO MC	8,024,824,168.00	55	79,783,432,178.00	98	41,533,337,757.00
13	BABATI TC		66		109	

		5,457,327,000.00		24,004,936,770.00		3,940,928,211.00
14	TARIME DC	32,869,616,373.00	99.95	9,864,355,980.85	75	19,233,168,225.00
15	MBOZI DC	18,607,938,847.00	148	58,091,697,722.00	104	9,736,560,676.00
16	DODOMA CC	89,183,261,252.00	104.5	79,167,620,178.00	110	65,802,561,040.00
17	GEITA MC	7,318,248,772.00	83	1,971,969,868.00	110.61	19,975,378,323.20
18	MWANZA CC	10,326,765,178.00	122	81,587,608,462.00	109	25,797,517,226.00
19	KALIUA DC	15,118,160,741.00	141	30,471,211,904.00	90	8,574,512,524.00
20	SHINYANGA MC	3,825,669,378.20	80	19,756,525,041.00	81	6,433,666,206.00
21	SINGIDA MC	36,164,182,143.00	103	26,593,050,903.00	103	5,981,265,311.00
22	UVINZA DC	10,259,596,343.00	74	25,280,214,750.00	105.36	4,059,991,000.00
23	NKASI DC	14,858,790,689.00	117	29,786,717,989.00	114	3,915,957,927.97
24	TANGA CC	11,801,081,904.00	114	50,234,687,602.00	109	15,021,383,800.00
25	MUSOMA MC	7,988,096,355.00	110	22,938,352,080.00	100	4,515,164,690.00
26	BAHI DC	8,378,939,152.00	118	22,378,941,397.00	105	2,134,706,568.00
27	GAIRO DC	7,576,041,000.00	75	19,550,858,418.00	96	2,004,082,254.00
28	IRINGA DC	21,194,965,355.56	126	3,180,502,128.00	85	5,581,067,392.00

29	IRINGA MC	5,453,320,402.00	67	37,205,687,227.00	100	7,504,193,067.00
30	ITIGI DC	6,556,524,388.00	77	14,903,329,120.00	95	2,640,339,727.00
31	MVOMERO DC	9,548,856,732.00	97	46,535,449,830.00	105	5,158,002,567.00
32	BAGAMOYO DC	4,388,387,001.00	55	30,398,968,813.00	93	7,731,629,401.00
33	BUKOMBE DC	13,615,179,105.62	100.87	33,891,854,333.00	100	3,731,634,715.78
34	BUNDA DC	13,504,617,708.00	148	24,632,211,300.00	99	2,195,383,847.00
35	KASULU TC	7,379,611,050.00	85	23,038,014,500.00	99.7	4,040,216,541.00
36	KIBAHA DC	9,293,612,630.00	94	26,566,361,862.00	106	4,698,859,156.00
37	KIBAHA MC	10,092,413,750.00	71	40,285,424,629.00	99.8	24,465,685,810.00
38	KIGAMBONI MC	6,601,141,308.00	79	34,558,389,028.00	113	18,253,180,098.00
39	KISHAPU DC	41,060,207,447.00	97	31,268,023,145.00	100	4,084,700,069.00
40	LIWALE DC	5,872,580,379.00	92	15,955,000,092.00	98.26	6,295,661,708.00
41	MADABA DC	6,373,871,521.00	86	10,396,253,207.00	87	1,696,675,542.00
42	MANYONI DC	6,916,671,179.00	95	20,986,992,666.00	100	3,491,911,893.00
43	MOSHI DC	12,952,929,966.00	69	60,567,152,896.00	98	4,377,175,831.00
44	MOSHI MC	41,571,097,964.00	92	35,143,919,796.00	99.7	9,123,183,925.00
45	MUHEZA DC	10,496,807,804.00	99	30,934,702,300.00	100	2,570,106,318.00

46	NAMTUMBO DC	12,116,894,506.00	132	25,124,857,724.00	100.2	4,165,862,304.00
47	PANGANI DC	5,613,174,979.00	68	11,206,412,760.00	96	1,843,492,751.00
48	RUANGWA DC	9,585,177,220.00	117	21,887,928,696.00	95.86	7,172,821,741.13
49	SAME DC	14,571,171,276.00	121	37,968,979,329.00	101	3,680,166,753.00
50	SONGEA MC	10,384,069,560.24	103	41,682,240,455.00	107	7,685,778,165.00
51	TABORA MC	17,305,902,683.00	136	36,234,468,200.00	90	6,447,648,334.00
52	TUNDUMA TC	6,244,526,635.00	84	17,750,295,212.00	63	15,653,557,412.00
53	ARUSHA CC	30,834,126,161.00	83	57,442,810,044.00	98	41,165,396,307.00
54	ARUSHA DC	12,753,529,498.00	111	58,019,274,935.00	103	6,407,649,432.00
55	BUHIGWE DC	10,178,019,023.00	97	20,933,526,125.00	99.9	1,877,535,327.00
56	ILEMELA MC	8,507,670,091.06	95	50,559,486,000.00	100	13,853,985,424.00
57	KASULU DC	7,746,690,174.00	80	22,416,494,315.00	100	3,935,787,147.00
58	KILWA DC	35,630,168,294.00	99	25,469,977,562.00	100.7	9,602,199,933.74
59	MAKAMBAKO TC	6,458,177,339.00	86	22,506,679,293.00	102	4,131,218,910.00
60	MASASI DC	13,397,395,080.81	120	27,862,573,613.00	104	8,440,199,563.00
61	MBEYA CC	9,401,801,276.00	89	67,494,828,500.00	109.67	24,999,581,635.00

62	MBEYA DC	11,270,069,892.00	91	53,074,749,962.00	107	7,301,584,567.00
63	MERU DC	12,622,549,462.00	104	52,076,608,773.00	108	7,585,723,249.00
64	MISUNGWI DC	11,061,813,952.35	115	47,503,821,906.00	100	4,022,887,950.00
65	MLELE DC	2,992,301,898.00	51	9,313,713,796.00	95	3,263,693,212.00
66	TANGANYIKA DC	6,535,890,982.00	73	19,235,369,840.00	105	9,145,855,240.00
67	MPIMBWE DC	6,184,491,056.00	89	12,555,169,276.00	101	4,207,263,602.00
68	MTWARA MC	6,974,832,672.00	88	20,532,525,055.00	104	7,760,989,283.00
69	NACHINGWEA DC	9,401,468,620.00	46.8	26,756,720,212.00	101.5	4,933,055,662.24
70	NJOMBE DC	9,272,433,814.00	107	19,102,380,242.00	99.97	5,080,201,398.00
71	NJOMBE TC	6,108,374,648.00	79	29,296,715,613.00	103	10,759,474,675.00
72	RUNGWE DC	11,844,427,256.00	111.45	48,039,802,088.00	106.26	8,067,920,978.00
73	SENGEREMA DC	12,833,507,138.00	75	45,068,625,646.00	98	3,165,282,106.00
74	TANDAHIMBA DC	8,312,929,350.00	71.3	28,710,471,906.00	97	9,177,161,224.00
75	UKEREWE DC	15,452,928,460.70	106	37,836,887,679.82	108	3,909,888,643.00
	JUMLA	**1,003,696,991,488.89**		**2,451,395,801,464.67**		**670,696,398,170.37**